# UTANGULIZI WA KITABU CHA YEREMIA
627-586 K.K.

Inawezekana Yeremia asiwe kama Isaya,lakini yeye ni wa kwanza katika moyo wa huruma, wa kusikitikia watu wake, na kupenda taifa lake na kujitoa kwa Mungu.

## I. MAANDISHI YAKE YANAHUSIKA NA UNABII, MASIMLIZI NA MAOMBOLEZO.

A. Kutabiri kuhusu kuteswa kwa Yuda na Yerusalemu.
B. Masimlizi yanaelezea kutimilika kwa haya katika kushuka na kuanguka kwa taifa la Kiyahudi.
C. Wimbo wamaombolezo unahusiana na kipindi mji wa Yerusalemu ulivyoanguka.

## II. UTUNZI KAMA HUU HAUSOMWI. KWA NINI?

A. Namna ya kuandika kwake kunaonyesha kwamba alikuwa mtu mwenye akili timamu, na mwenye huzuni.

1. Mtu anayejulikana kama " nabii wa maombolezo" hawezi kupendwa na wengi.
2. Alikuwa na agizo lenye jitihada.
3. Alikuwa mjumbe wa kutangaza maafa au maangamizi
4. Ni yeye tu aliyetabiri kurudi kwa wana wa Israeli baada ya miaka 70

B. Urefu wa maandishi haya:

1. Ni karibu 1/20 ya biblia nzima.
2. Kitabu hiki kina habari kuhusu kipindi kigumu walimoishi watu wale mwokozi angelitoka kati yao.
3. Maonyo yaliyomo ndani yanatufaa hata leo.
4. Sura hizi ni ngumu kuzisoma kwa sababu hazijapangwa kwa kufuata matukio.

## KIPINDI ALIMO ISHI YEREMIA (2 Wafalme 22-25 &2Nyako 34-36)

**A. Tunayoyaona ni upotofu na kukosa utaratibu. Katika mambo ya usuli tunaona miji inayoungua, na majeshi yanayopigana, na safu za majeshi mateka, ukiwa na maangamizi ya mji.**

2. Kinacho onekana waziwazi ni Yerusalemu, kutojutia makosa, kutokuwa na msimamo na upofu Kuhusu maafa , yaliyotabiriwa.

3. Katika malango ya miji, na ua, la hekalu kuzungukwa na kundi la maadui, anasimama nabii asiyependwa akiwatangazia maonyo na maangamizi yanayokuja.

B. **Matengenezo aliyokuwa amefanya Hezekia, yameondolewa na**

**ukengeufu wa Manase mwanawe**.

1. Kipindi cha miaka 55 cha utawala wa Manase kimezidi machukizo ya ibada ya sanamu, na kuanza kutesa waabudu wa kweli.

2. Baadaye maishani mwake Manase walipokuwa wamepelekwa Babeli alitubu,lakini alikuwa amechelewa kuokoa watu wake.

3. Manase alifuatwa na mwanawe Amoni aliyefuata tabia za Babaye.

**C. Yosia mwana wa Amoni alikuwa mfalme aliye fuata.**

1. Mtawala mzuri huyu aliangamiza ibada ya sanamu; baada ya kukipata kitabu cha sheria Hekaluni.

2. Aliwauawa na Niko wa Misri vitani

**D. Yehoyahazi aliyeitwa pia Shallumu**.

Baada ya kutawala kwa miezi 3 aliondolewa na Neko na kumpeleka uhamishoni Misri alikofia.

E. **Jehoyakimu kaka yake alichaguliwa badala yake na mfalme wa Misiri**.

1. Niko aliposhindwa kule Karkemishi na Nabukadreza, alikuwa chombo Cha ushindi wa Babeli.

2. Katika kipindi cha miaka 11 cha utawala wake, watu waliangamia katika Ibada ya sanamu zaidi.

3. Alimwasi Nebukadreza na kufukuzwa asiwe mtawala.

**F. Yehoikini-aliyeitwa pia Yekonia au Konia alitawala badala ya Babaye.**

1. Alifuata nyayo za Baba yake.

2. Alitawala miezi mitatu tu na kupelekwa uhamishoni Babeli na kukaa kule kama mfungwa kwa miaka 37.

3. Wakati wa kupelekwa kwake watu wenye ujuzi na wasomi walipelekwa pamoja naye.

4. Yerusalemu ikaachwa ukiwa na kubakia na kivuli cha utakufu wake wa kale.

**G. Kama mfalme asiye na mamlaka zedekia aliyekuwa ndugu,**

yake alianza kutawala ndugu.

1. Katika njama yake yakipumbafu kwa kushirikiana na misri aliasi Babeli. Nebukadreza akauhusuru mji na Kuuangamiza.

2. Zedekia akakokotwa hadi Ribla, waliko wa ulia wanawe mbele ya macho yake.

3. Baadaye macho yake yalitobolewa na kupelekwa Babeli na kuweka jela.

4. Hapo ndiyo mwisho wa utawala wa miaka 400 wa wafalme katika Yerusalemu.

5. Baada ya haya Gedalia alichaguliwa na Nabukadreza kuwa liwali waYuda.

   a. Alikuwa na Ishimaeli Myahudi wa ukoo wakifalme na kufuatiwa na mchafuko.

   b. Kundi dogo la wakimbizi lilikimbilia, Misri.

**IV. Maisha ya Yeremia yalichukuwa urefu wa kipindi cha wafalme 5 wa Yuda.**

A. Alizaliwa kama mmoja wa familia ya makuhani katika mji mdogo Uliyoitwa Anathothi maili 3 kaskazini mashariki mwa Yerusalemu.

B. Aliitwa kuwa nabii akiwa mtoto mdogo.

1. Ulikuwa katika mwaka wa 13 wa utawala wa Yosia-626 K.K

2. Mwanzoni aliogopa kazi.

3. Alikatazwa asiowe au kwenda katika nyumba yenye, sherehe.

4. Akiwa amesimama peke yake alijikuta anapingwa na watawala, watu, manabii wa uongo na makuhani.

5. Kokote alikoonekana alichukiwa, alidharauliwa,aliogopewa alitishiwa.

6. Licha ya hayo yote alitoa ujumbe wa Mungu akiwa na moyo udondoshao damu(moyo wa kuwalilila).

7. Njama ilitengenezwa dhidi ya maisha yake na watu wake wenyewe.

V. **UJUMBE WA YEREMIA**.

A. Kila aina ya jamii ya kiebrania walitiwaa hatiani bila udhuru.

B. Kwa sababu Yuda walikataa kutubu, kupelekwa uhamishoni lilikuwa ni jambo lisilopingika.

C. Wayahundi wote walitakiwa kunyenyekea chini ya kongwa la Wakalidayo
Bila kuasi kwa kuwa ilikuwa ni adhabu kutokana na kutokuwa waamiuifu katika Agano la Mungu.

D. Lakini siku ingefika kwa Isaeli kukombolewa na Masihi.

E. Mwisraeli halisi alitakiwa kumtumainia Mungu sio katika silaha za mwili. Mkristo naye kama mtu wa Mungu anapaswa kuwa hivyo.

F. Yeremia ndiye nabii wapekee aliyetaja kipindi cha miaka sabini cha Utumwa wa kule Babeli.

## VI. YEREMIA KAMA MTU.

### A. Mafunzo yake ya awali.

1. Alilelewa katika mji wa Anathothi (karibu na Yerusalem).

2. Aliingizwa katika kundi la wasomi, makuhani, manabii na wanafunzi wa neno la Mungu alipokuwa akikua.

### B. Kuitwa kwake.

1. Alikuwa,mwoga, na mwenye aibu –lakini alikuwa tayari

3. Mungu alimwita na kusema, atakwenda kumtuma, kumwamuru na kuwa pamoja naYeremia

4. Alifanya unabii kutoka mwaka wa 13 wa utawala wa Yosia hadi mwaka wa 11 wa utawala wa Sedekia.

### C. TABIA YAKE.

1. Alikuwa mwenye huzuni sana.

2. Hakueleweka vizuri na watu wa familia, kiasi cha kumkataa. Alipingwa na makuhani na manabii. Maisha yake yalikuwa maisha yaliyojaa matatizo.

3. Daima aliwasihi wananchi wenzake kumrudia Mungu.

4. Alikuwa na elimu nzuri.

**D. DINI YAKE.**

1. Ilikuwa ni habari moyoni mwake mwenyewe
2. Alimtegemea sana yule aliye wa milele.
3. Alikuwa na mtazamo wa kiroho kuhusu dhambi uliokuwa tofauti na manabii wengine.

**7.MASOMO TUNAYOYAPATA KATIKA KITABU CHA YEREMIA.**

A. Moyo wa Mungu ulio laini huumia sana unapotazama watu Wake aliowachagua wanaposahau vyapo vya siku zao za mwazo.

B. Toba sahihi lazima itangulie kutolewa, kwa baraka za Mungu Maishani mwa mtu,binafsi.

C. Dini ya kweli ni ile ilio ya ndani, ya kiroho, yenye moyo wa utii, mkamilifu kwa haki ya Mungu.

D. Dini inaweza kujaribiwa na matokeo yake katika kuzaa tabia Njema.

E. Dhambi haiwezi kushinda Mungu lazima awe na ushindi juu Yake.

F. Kila mtu anasimama peke yake mbele ya Mungu mwenye haki. Na anapaswa hukumiwa kama mtu binafsi.

G. Agano jipya hutoa utendaji wa Mungu (usio wa kimiujiza) juu ya moyo Ili maisha yathibitishwe.

H. Mhudumu anayeteseka sana na kuegemea sana kwa Mungu na neno lake ni yule anayejua kwa kina ukweli wa Mungu.

I. Daima matokea ya dhambi ni maangamizi Hukumu haiepukiki, ni ya lazima na ya milele.

**VIII. MANABII (RUM 15:4)**

A. **Afisi ya unabii hutolewa na Mungu** (Kumb.18:9-22) manabii Walikuwa wanaume walioinuliwa na Mungu. Katika vinywa vyao

Mungu aliweka neno lake. Walisimama kinyume na wasihiri wa kule Kanaani. Israeli walitakiwa kuwasikiliza manabii wao. Sio watu Wengine

B. **Kazi yao:**

1. Kuwaelezea Israeli neno la Mungu. Walitabiri wakati ujao Lakini zaidi walitangaza ujumbe kutoka kwa Mungu.

C. **Manabii walikuwa walimu wa kipindi cha Agano la kale (pamoja na makuhani) Yeremia 1:8,9.18.11**

1. Wanaume na Wanawake wenye hekima kwa mashauri (2Sam.14:1-24,2 Sam,20;16-22) Sulemani na wengine.

D. **Baadhi ya maneno ya Agano Jipya kuhusu manabii.**

1. Walinena kutoka kwa Mungu (2Pt.1:20-21).

2. Wote walitabiri kuhusu wakati wa sasa (kipindi cha Ukristo) (Mdo.3:18 ,22-26)

3. Yalisomwa kila Sabato (Mdo 13:27).

4. Waliteswa na wasikilizaji wao (Mdo.7:52;Mt 23:37Neh. 9:31).

5. Paulo alipingana na manabii wa uongo na kuwashinda (Mdo.28:23).

6. Wameunganishwa na injili (Rom16:25-27,Lk.24:27).

7. Hata kurudi kwa Kristo kuli tabiriwa (Yuda 14-16).

E. **Maana ya neno nabii:** Nabii ni mtu yule ambaye akiwa chini haongozwi na Roho Mtakatifu, huzungumza maneno, na mawazo ya Mungu; Hata kama yanahusu wakati uliopita, wa sasa, au ujao. Nabii ni msemaji wa Mungu. Maneno, yake hayatokani roho yake mwenyewe, bali yanatoka katika chimbuko la Juu.

1. **Majina mengine walioitwa** : **mwonaji** (1Sam.9:9) **Mtu wa Mungu**, (1Sam.9:6,) **Mtumishi wa Mungu**. (Isaya 20:3,) **Mjumbe wa Yehova** (Isaya 12:19) **Mlinzi.** Ezekieli 3:17)

2. Kuna aina mbili ya wahubiri, wahubiri wazuri walio na kitu cha kusema,na wahubiri wabaya wanaosoma chochote. Kikundi cha tatu na cha juu ni nabii, aliye na cha kusema na kwa hiyo anakisema.

**F.** **Manabii waliosema bila kuwa waandishi ni: Ibrahimu**, (Mwanzo 20:7,17. **Isaac** na **Yakobo** Zaburi 105:9-15, **Musa**, kumbu. 18:15,34:10, **Miramu** kutoka 15:20 **Deborah**, Waamuzi 4:4, **Eliya** 1Wafalm 17:24,**Wana wa manabii** 2 Wafalme 2:3.

**G.** **Umoja bila kufanana**:

Amosi--- alikuwa Machangaji

Mika---alikuwa mtu wa mashambani

Zekeria- alikuwa mtu wa ukoo wakifalme.

Zekeria-Alikuwa Kiongozi wa watu wake

Sefenia alikuwa kijana lakini Haggai alikuwa mzee. introspective

Habakkuki alikuwa mtu wa taadhari na mwenye kutafakari, lakini Nahumu alikuwa radi.

**H.** **Utaratibu wakimsingi wakuwafahamu manabii**

1. Nabii alikuwa mtu anayeongozwa na Roho Mtakatifu (Pt1: 20, 21).

2. Nabii hakuweza kuleta dini ya kigeni (Kund.13: 1-5). Manabii hawakuleta Sheria mpya, bali kazi yao ilikuwa kuwaita watu wairudie sheria aliyopewa Musa bila kubadilisha. (Gal 1:6-9).

3. Nabii wa uongo ni yule ambaye maneno yake hayatokei (Kumb.18:20-22)

4. Unabii ulikuwa na masharti (Yereumia 18:5-10).Swali linalopaswa Kuwekwa mbele ni hili: Je! mashariti haya ameyatimiza? Mungu hakuiangamiza Ninawi mara moja licha ya vitishio vya mara kwa mara vya Yona akitaka watubu.Vitisho vinaweza kucheleweshwa na toba; (1Wafalme 21:29)

5. Manabii walioishi kabla na mara baada ya utumwa wa Ashuru na Babeli Vitisho vya maangamizi Zakeria anawa kumbusha waliotoka utumwani kwamba vitisho dhidi ya baba zao vimetimizwa (Zakara 1-5-6).

6. Kuja kwa Kristo na kuanzwa kwa kanisa ni somo muhimu la unabii wa Agano la Kale (Rum.1:1-4;1Pt.110-12)

7. Ufunuo wa Mungu wa Mwisho ameufanya kupitia mwana (Ebrania
   Ni kwa sababu ni waandishi wa Agano Jipya husema, “Lakini jambo hili
   Ni lile lililo nenwa kwa kinywa cha nabii Yoeli (Mdo2:16).

**IX, Unabii wa Biblia uliotumika----Je ni jambo lililotokea tu kwa nasibu?**

**A. Unabii ni nini?**

1.Manabii katika Biblia walikuwa wasemaji wa Mungu.
   (a) Alituma mawazo kwa njia ya watu aliowachagua.

   (b) Tabiri (toa unabii) “tangaza,”

2. Watoa ujumbe wa Mungu .

3.Wakati mwingine walielezea mambo yajayo.

**B. Alama za nabii wa kweli ni zipi?**

1.Wakati kamili (mapema kabla ya kutendeka?

2.Mambo yenyewe kamili.

3.Unabili wake usilete Utata.

4. Ukamilifu Kamili.

5. Wakati halisi.

**C. Mifano ya unabii uliotimilika ni ipi?**

1. Babeli moja ya miji mkuu wakati wote.

   a. Sifa za sasa: Kilimo cha umwagiliaji, barabara za lami, nyumba za gorofa, njia za mitaani zenye mataa, bomba za maji. Kuta pana za kutosha magari matatu ya farasi kupita juu yake. Bustani za kuning’inia za Babeli.

   b. Ibada ya sanamu yake na kuingilia Israeli na kuanza kuwatesa watu wa Mungu kulimfanya Mungu kutangaza maafa kupitia nabii Isaya katika mwaka wa 700 K.K. (Isaya 13:19-20)

   c. Miaka mia moja baadaye Yeremia alitabiri kuanguka kwa Israeli, akisema kwamba atatumikia mfalme wa Babeli kwa

miaka 70 (Yeremia 25:11) Pia kuhusu ukiwa wa Babeli (Yeremia 25:12-14)

d. Wamedi wakiongozwa na Koreshi walishambulia katika mwaka wa 539 K.K. Baadaye ulitekwa na Ahasuero na Iskanda Mkuu.

e. Mabaki ya mji yalisababisha kemikeli katika ardhi na kufanya ardhi hiyo kuwa ukiwa.

f. Katika karne ya kwanza harufu ya uvundo ulisababisha mabaki kuwa makazi ya wanyama pori tu.

g. Ilikuwa vigumu kuufikia mabaki ya mji wa jumba la kifalme kwa sababu ya wingi wa nyoka wenye sumu kali na nge.

h. Waarabu hawapendi kuona jua likizama katika eneo lile.

2. Tiro mji tajiri na wenye maendeleo mazuri pwani mwa Bahari Kuu.

a. Walijivunia kuta zao zisizoonekana za futi 150.

b. Walimkosea Mungu kwa sababu ya kiburi chao na mateso walio wafanyia wafungwa wa vita wa Kiyahudi, walivunja agano na mfalme Sulemani. (Amosi 1:9,10)

c. Katika karne ya sita Ezekieli alitabiri maangamizi yao.

1. Mji ungelivunjwa
2. Na kugeuka mahali pa wavuvi kutandazia nyavu zao.( Ezekieli 26:3, 14,9)

d. Nabukadreza aliuhusuru kwa kipindi cha miaka 13 na kuharibu mji. Watiro walikimbilia upande wa kisiwani karibu nusu maili kutoka pwani (332 K.K.) Iskanda aliungilia na kuharibu mabaki yake. (Kutimilika katika Ezekieli 26:12)

e. Uliangamizwa kabisa katika karne ya 13 na Waislamu.

f. Siku hizi watali wanatazama wavuvi wakizitandaza nyazu zao juu ya majabali makavu.

3. Edomi waabudu miungu na watesi wa Israeli (Isaya 34:5-12; Amosi 1:11, 12; Ezekieli 25:14)

a. Uliharibiwa na majeshi ya Wamakabbayo katika mwaka wa 164 K.K. na kumaliziwa katika 120 K.K.

b. Katika mwaka wa 70 W.K. Rumi walipokuwa wakiangamiza Yerusalemu, Waedomi walitoweka na nchi ya Waedomi kubakia maame.

4. Ninawi: Mji mkuu wa Ashuru.

a. Mungu aliwapa nafasi ya kutubu kupitia mahubiri ya Yona.

b. Baadaye walirudia tabia yao ya ukatili na uaji.

c. Katika karne ya saba ……unabii dhidi ya mji huu (Nahumu 1:1-8, 2:3-6)

d. Katika 612 K.K. Jeshi la Babeli na Medi walichepusha mto Tigra(Hidekeli) na kusababisha mafuriko kuangamiza kuta na majengo ya mji kabisa. (Nahumu 2:6)

e. Katika Nahumu 3:7 "…..Ninawi umeharibika ni nani atakaye kuhurumia?…

**C. Baadhi ya unabii kuhusu Kristo kama Masihi uliotimilika ni upi?**

. 1. 333 K.K.---UTABIRI WA AGANO LA KALE KUHUSIANA NA MASIHI?

2. UNABII UNAANZIA KATIKA KITABU CHA MWANZO 3:15

3. YESU MWENYEWE ALITOA UTABIRI MWINGI.
   A. ALITANGAZA KUSULUBISHWA KWAKE MIAKA MITATU KABLA (YOHANA 3:14)
   B. ALITANGAZA KUFUFUKA MIAKA MITATU KABLA (YOHANA 2:19,21)
   C. KUANGAMIZWA KWA HEKALU LA YERUSALEMU (MATHAYO 24:2)

**D. NI VIPI KUHUSU UNABII WA ISRAELI?**

1. KUTAWANYIKA KWA WAYAHUDI. (KUMBU. 28:64-68)

   A. KARNE 15 BAADA YA UNABII WA MUSA (70 W.K. YERUSALEMU ULIANGUKA.
   B. WALIOPONA ZAIDI YA MILLION 17 WALIKIMBILIA MISRI

2. UTABIRI KUHUSU KURUDI( ISAYA 43:56; YEREMIA 29:14)

A. MIAKA 1800 WAYAHUDI WALIANZA KURUDI
B. 1935 ZAIDI 300,000 WALIKUWA PALESTINA
C. 1936 ZAIDI MASHAMBA EKARI 350,000 YALIKUWA TAYARI WAMENUNULIWA .
D. 1949 UMOJA WA MATAIFA ULIKUBALI ISRAELI KAMA TAIFA
E. BADILIKO LA ARDHI KUTOKA UKIWA NA KUJENGA MIJI YA KISASA (ISAYA 51:3; ISAYA 61:4; EZEKIELI 36:34,35)
F. USHINDI DHIDI YA MATAIFA YA KIARABU KATIKA MWAKA WA 1948 NA 1967)

UNABII ULIOTIMILIKA HAUTHIBITISHI KUWA MAANDIKO YALIVUVIWA BALI YANATHIBITISHA KUWA BIBLIA NI KITABU KILICHOANDIKIWA NA NGUVU ZAIDI YA UWEZO WA KIBINADAMU.

MUHUTASARI WA YEREMIA

I. UNABII CHINI YA UTAWALA WA YOSIA NA YEHOIAKINI……………SURA 1-20

II. UNABII WA BAADAYE CHINI YA YEHOIAKINI NA ZEDEKIA…………SURA 21-39

III. UNABII BAADA YA KUANGUKA KWA YERUSALEMU……………….SURA 40-45

IV. UNABII KUHUSU MATAIFA YA KIPAGANI……………………..…….SURA 46-51

V. KIUNGO KINACHOHUSU HISTORIA………………………………….SURA 52

MUHUTASARI WA YEREMIA ULIOPANULIWA

I. UNABII CHINI YA UTAWALA WA YOSIA NA YEHOIAKINI……………SURA 1-20

A. KUITWA KWA NABII………………………………………….SURA 1
B. DHAMBI NA KUTOSHUKURU KWA TAIFA 2:1-3:5
C. UTABIRI KUHUSU KUHARIBIWA KWA KASKAZINI 3:6-SURA 6
D. TISHIO LA WAUHAMISHO WA BABELI SURA 7
E. AGANO LILILOVUNJWA NA MKANDA…………….SURA 11-13
F. UKAME, ISHARA YA NABII ASIYEOA………………….SURA 14-17
G. ISHARA YA MFINYANZI………………………………SURA 18-20

II. UNABII WA BAADAYE CHINI YA YEHOIAKINI NA ZEDEKIA…………SURA 21-39

A. NABUKADREZA CHOMBO CHA MUNGU CHA KUMWADHIBU ZEDEKIA NA YERUSALEMU……………………………………….SURA21-29

B. UFALME WA KIMASIHI UJAO……………………………SURA 30-33

C. DHAMBI YA ZEDEKIA NA UAMINIFU WA WAREKABU……SURA 34,35

D. UPIZANI WAYEHOIAKINI NA KUANGAMIZA MAANDISHI YA KIUBANABII…………………………………………………..SURA 36

E. YEREMIA GEREZANI WAKATI WA KUHUSURU……………….SURA37-39

III. UNABII BAADA YA KUANGUKA KWA YERUSALEMU……………….SURA 40-45

B. HUDUMA KATI YA MABAKI YA YUDA……………………….40-42

C. HUDUMA KATI YA WALIOKIMBILIA MISRI…………………...43,44

D. KUTIWA NGUVU NA BARUKU……………………………….SURA 45

IV. UNABII KUHUSU MATAIFA YA KIPAGANI……………………..…….SURA 46-51

A. MISRI………………………………………………………SURA 46

C. WAFILISTI………………………………………………..SURA 47

D. MOABI……………………………………………………..SURA 48

E. AMONI, EDOMI, DAMESKI, ARABIA, ELAMU………………….SURA 49

F. BABELI……………………………………………………..50,51

V. KIUNGO KINACHOHUSU HISTORIA………………………………….SURA 52

## YEREMIA KWA UFUPI.

**JINA: Yeremia**

**MAANA: Yehova huchagua.**

**TAREHE: 600K.K.**

**WASIKILIZAJI: Yuda.**

**WAZO LA KITABU CHA YEREMIA: Lazima Yuda ianguke.**

HABARI MAALUM: **Agano Jipya linakuja** (31:31-ff).

MHUTASARI MFUPI:

I. Unabii kuhusa Yuda …………………………………..SURA 1-45

II. Unabii Kuhusu mataifa ya siomjua Mungu……………..SURA 46-51

III.Kipande cha Kihistoria ………………………………...SURA 52

MASOMO:

1. Mungu anachagua anayempenda kufanya kusudi lake hapa duniani.
2. Mungu daima hushikilia mshale wa nuru wenye matumaini.
3. Ishi kama mnyama utakufa kama mnyama,
4. Sala za wasio male Mungu hazisikilizwi.
5. Dhambi zetu hutushuhudia.
6. Ahadi zote za Mungu ni zenye mashariti
7. Amelaaniwa yule afanyaye kazi ya Mungu kwa ulegevu.

**Ufupisho wa kitabu 1:16**

I. Unabii kipindi cha Yosia na Yehoiakinu SURA 1-20

**A. Wito na agizo la nabi ………………SURA I**

**SURA 1**

**Yeremia atakiwa na Mungu Kupinga kila wazo litakalo mwekea Mungu mipaka ya Nguvu zake.**

2,3. Yehova ametangaza mwisho wa utaratibu wa ulimwengu kama Yuda wanavyojua. Kutenganisha kwa utawala wa kifalme, kudhoofisha utaratibu wa uma pamoja na raia kutokuwa na imani, havitokani na Mungu kukosa nguvu za kutawala. Kile ambacho kingeonekana kuwa udhaifu upande wa Yehova ni utaratibu wake alio uandika katika sheria.

Kwa sababu sasa Mungu amezungumzia maangamizi, Yatakayotokea, Kinachotakiwa ni kusubiri na kutazama na kuona,yakitimia. Kitabu hiki cha Yeremia Kina hadithi ya kusubiri na kutazama utimilifu wa maneno yote

5. Mungu humchagua yule amtakaye kufanya mapenzi yake hapa duniani
Cf. Gal 1:15,16 (Saul/Paul).

6. Ingawaje kukataa kwa Yeremia kunatukumbusha kule kwa Musa ,lakini si sawa. Musa alijisikia hawezi kusema, lakini Yeremia alijiona kuwa yeye hana sifa, au hakuwa tayari na ya kwamba hana ujuzi.

7.Uwe mwanaume.

Watu wa Mungu wasiwe watu wakurudi nyuma na kutokuwa karibu na Mungu katika maisha yao ya kila siku. Wanatakiwa wawaendee watu wakiwa na ujumbe kutoka kwa Mungu.

Uoga kama huu ni mzuri kwa sababu ndani yake tunajiona kwamba hatuwezi bila Mungu (1 Kor2: 3) Lakini tukiwa na ufahamu kwamba, tunaweza kumfanyia Bwana makuu.(Filip 4:13)

9,10. Kile kitakachofanywa na neno la Mungu, (Kumb 32:39,Isaya 55:11,14:24-27

11,12. Mti wa mlozi uliitwa “Amka”.kwa sababu mti huo ulikuwa wa kwanza kuota na kutoa maua yake. Na hii ilikuwa hata kabla ya kuweka majani yake. Yehova anasema,“nimeamka na kwa hiyo nafahamu kile ninachokisema na kwa hiyo nitakifanya. - Isaya 55:11

13,14. Sufuria lenye maji yatokotayo kutokea Kaskazini.

16. Msitari huu ni muhutasari wa unabii huu. Uhusiano wa Israeli na Yehova ulitegemea neema yake na ahadi zake. Lakini Mungu alihitaji imani na utii kutoka

kwa watu wake. Uovu wa Yuda lazima utaadhibiwa.

17-19. Wewe fanya upande wako na mimi nitafanya Upande wangu.

. Yeremia kama mtu anayeyuka katika machozi na katika huruma kama mbebaji wa neno la Mungu. Ni imara na mgumu kama nguzo na kuta, hata dhuruba ya hasira ya mataifa wanajaribu kuvunja lakini wanashindwa. Nabii wa kweli wa Mungu hawezi kusema, "Mambo yote ni swari" Yehova hutuma nabii kwa watu wake wanapokuwa katika matatizo naye ili kuwarudisha kwake.

**B. Dhambi na kutoshukuru kwa taifa…………………………… 2:1-3:5**

**SURA 2.**

Yeremia kama wahubiri wengine wa kweli, anayo mawazo kadha yenye ukomo anayohubiri. Anazihubiri akizirudia rudia kwa bila kusita, akiwa na huruma.

Sio kwa sababu Mungu amepoteza nguvu anapowacha watu wake. Ni kwa sababu hataendelea, kuwalinda watapokuwa wameacha kumtumikia na kuanza kutumikia miungu.

2. Mwanzoni Israeli walikuwa waaminifu- (Ufu. 2:4,5).

3. Watu wa Mungu ni wake:

(a) Watakatifu kwake.

(b) Malimbuko

Yeyote nayeshambulia mtu wa Mungu ni:

(a) Mwenye hatia na

(b) Uovu Utakuja juu yake

1. Wakati mwingine yatamfikia katika ulimwengu huu.
2. Lakini daima katika umilele.

Kila **"alaye"kilicho cha Yehova** ana hatia ya dhambi na kwa hiyo ataadhibiwa

5. Mungu anauliza Isreli, "Nimakosa gani waliyo yaona kwa Yehova Yaliyo wafanya wamwache?

Sanamu = utupu.

Waabudu sanamu = Bure.

Wazo ni kwamba Israeli walifuata miungu ambayo ni “bure” kwa sababu tu ni Kuchukuwa tabia ya kile tunacho kipenda na kukiabudu, Israeli nao wamekumbwa (Hosea 9:10; Zaburi 115:18

6,7. Agano walipewa watu walipokuwa jangwani wakati hali ya maisha ilikuwa mbaya.

8. Wayahudi kama walivyo watu wengine, wamepofuka wasione dhambi zao wenyewe. Kwa sababu sasa wamefanikiwa wamesahau maagano na Kuyavunja.Yeremia alipaswa Kuangamiza utulivu wao. Walihudhuria kwa wingi huduma zao za kidini, lakini hawakuwa sahihi na Mungu.

Aina tatu ya vikundi vya kulaumiwa:

Makuhani: Walikuwa ndiyo walimu wa ufunuo wa Mungu kwa watu. Lakini hawa kumfahamu Mungu wenyewe. Kumjua Mungu ni kutii katika maisha ya kila siku, sio kuwa tu na ufahamu, wake,

Watawala- Walifaya kazi muhimu katika dini, siasa, na ustawi wa jamii wataifa. Hawa walikuwa wameshindwa. Tazama Zaburi 72 mfano wa kiongozi mzuri.

**Manabii-** Walikuwa manabii wa uongo. Wakidai kuwa wametokea kwa Yehova, Lakini wakizungumza walio yataka watu kusikia. Sio alichokita Mungu wasikie. Linganisha 1. Wafalme 13,22. Karibu daima taifa lisianguke ni kwa sababu Viongozi wameshindwa kutekeleza wajibu Mungu alwowapa.

9-11. Hata mataifa hawabadilishi miungu yao.

Israeli wamesahau historia yao. Pale historia ya nchi inaposahuliwa, Kupotea kwa nchi kutafuata.

Israeli walikuwa wamepokea neema nyingi kutoka kwa Bwana. Lakini walicho Kuwa wamesahau ni kwamba neema hiyo inadai mengi kwa wale walioipokea Inadai Imani na utii . Pasipo imani na utii neema hufanyika kuwa maneno matupu na kupoteza thamani yake.

.

13. Upambanisho umefanywa wenye nguvu zaidi –Dhambi mbili
(a)Kumwacha yehova na
(b)Kujichimbia mabirika

Yehova = maji yaliyo hai -yasiyo na mwisho –mazuri daima.
Mabirika = maji yaliyokufa –yanayokoma – mabaya daima.
(a) mabirika yote hupasuka
(b) hata yakirekebishwa –huwa na harufu ya udongo -yamejaa vidudu .
(c) yana kikomo na hayawezi kujizidisha. Linganisha Yohana 4:14.

Ni rahisi kwetu kuangalia nyuma na kutangaza kwamba Yeremia alikuwa Sahihi .Lakini je sisi pia si vipofu katika maisha yetu ya kila siku tunayo Yamalizia katika dhambi .Bila kufanya mambo yale Mungu anayotaka Tufanye?.Taifa la kiyahudi lililokuwa limemfahamu Yehova katika nguvu Na ukuu wake.walikuwa sasa wanaenda sambamba na wapagani

16. "nofu" "mephis" mji mkuu Misri ya chini.
"Tahpanesi" baadaye utaitwa "daphne"

18. Israeli wanapotafuta msaada kutoka mataifa mengine, hapo watakuwa wanamwacha Yehova. Yehova amekuwa mlinzi wao na Israeli wanasema, tunahitaji ulinzi tofauti na bora.

19. Dhambi za Israeli ndizo zitakapokuwa sababu yao ya kuanguka .Watatazama dhambi na kufahamu sababu ya kuadhibiwa kwao.Tatizo la Israeli lilikuwa la kidini .Yote yakisha zungumzwa na kufanywa, yote yanaelekea uhusiano au utengano wa kidini tulionao na Yehova. "BWANA MUNGU WAKO" – hii ni kusema kwamba wewe ni mali ya Mungu sio kwamba Mungu ni mali yako. Wakati mwingi tunaangalia katika upendo wa Mungu na kuuchukulia kimakosa kama upendo laini bila kujua kwamba upendo wake unadai mendi kutoka kwetu.

20. Maovu daima yana thamani yake iliyo chafuliwa.

23. "Katika bonde" -bonde la Ben-Hinnom lilikuwa nje kidogo mwa Yerusalemu kulitendeka vitendo vya kipagani vingi pamoja na kutoa watoto wao kama dhabihu ya kuteketezwa.(Yeremia 7:21-26; 2Wafalme 23:10)

24. Israeli amekuwa kama mnyama aliyefika kupandwa, madume hawamtafuti bali yeye amejiweka tayari kwa kila dume anayekuja.

25. Israeli atakwenda uhamishioni bila viatu akiwa na kiu.

27,28 Kama miungu wa uongo walikuwa wa kweli,

(a) Mti angelikuwa baba yao na
(b) jiwe angelikuwa mama yao.

Hebu na miungu ya uongo iwaokoe Israeli- Kila mji ulikuwa na miungu, kwa hiyo wangeliwatosha tu.

29-37. Huruma na ushirikiano wa Mungu ni wenye masharti. Unategemea uitikio Wetu .Imani yetu na utii wetu ukishindwa Mungu atasitiza huruma na Ushirika .

36. Ukengeufu wa kisiasa , kidini ,na watabia vinaenda sambamba
Wenye hatia mara mbili: –

(a) Kuabudu Miungu mingine .
(b)Uovu wa kitabia ulikuwa ufisadi , na kutotenda haki .

Mungu anapokataliwa thamani ya nchi kitabia huzorota na watu kubakia kutafuta kujifurahisha wenyewe.
Mungu hawezi kuruhusu mambo ya kidini kutenganishwa na sheria za Serikali zinazohusu watu.

37. “Kutoka mikono yako juu ya kichwa chako” = ni kuwa katika huzuni

SURA 3.

1. Kisheria mwanamke akishamwacha mume wake wa kwanza asingemrudia. Kwa hiyo nao wasingeliweza kumrudia Yehova bila toba kamilifu. Na hii Ingelichukuwa adhabu kali.
2. “Kama Mwarabu jangwani” Ungelitarajia mwanamke akiwa njiani kushambuliwa, lakini Israeli inatamaa sana na wapenzi ndiye anayetafuta waume.
3. Kipaji cha uso cha ukahaba = upara – wasiotaharika daima ni wajasiri.
6. Kuasi. = Ni ukengeufu

**C. Utabiri kuhusu maangamizi kutoka kaskazini .3:6-Sura 6.**

8. Israeli (kabila 10) wametalakiwa na Yehova.

10. Udanganyifu – ni katika kipindi cha Yosia.

11. Kwa nini Yuda ilikuwa yenye haki kuliko Israeli ! Yuda alikuwa na mfano wa Israeli mbele yake na bado anafuata njia ya maangamizi alioifuata Israeli.
13. Haiwezikani kuwa na upatanisho kati ya Mungu na mwanadamu –mwanadamu Asipoangalia kwa uaminifu sababu ya kutengana na kutubu kwa uhakika.

14-19. Mwanga wa tumaini,-- Mungu daima hushikilia tumaini.

18. Tumaini- kunapaswa kuwa na mwanga wa tumaini kwa imani kuendelea au kutiwa nguvu.

19. Ni picha ya baba aliyefanya kazi kwa muda mrefu na kumjengea mwana urithi. Wakati umefika wa kumpa mtoto wake urithi lakini mtoto hajali kuhusu urithi. Ameusahau .Mtoto amemkataa baba. Baba amehuzunika sababu ya hali ya mtoto Wake, lakini hawezi kumpa urithi wake.

22. Ni jambo la kukatisha tamaa kiasi gani kuhubiri toba kwa watu wanaojisikia kuwa tayari wametubu. Viongozi wao wa kidini wamewaambia kwamba wako katika hali nzuri na Mungu tayari. Lakini viongozi hawa walikuwa makosa! Mafundisho yao ya uongo yalikuwa yamewazuia kuona ukweli.

Haitoshi kutamani kutopata adhabu kutoka kwa Yehova, Unapaswa kuishi kwamba utapata thawabu kutoka kwake.

24. “Tokea ujana” maana yake ni kwamba toka mwanzo wa Israeli kama taifa, wametafuta mbadala wa Mungu wa peke, Yehova.

## SURA 4

Mst. 1-4. Tubu Yuda usiwe kama Israeli;
Ingawa wameuumiza moyo wa Yehova , bado anayo nafasi ya upatanisho.

4. (a). Tohara ilikuwa alama ya kufanya Agano na Mungu. Kama hakuna kujitoa kwa ndani kunaoenda sambamba na alama ya nje ni bure. Tohara itakuwa ya bure.
(b) Ubatizo ni alama ya kuonyesha kwamba mtu amekubaliana na mapenzi ya Mungu, kama kujitoa kwa mtu kwa ndani kusipoenda sambamba na alama ya nje, kubatizwa kwa mtu kutakuwa bure.

Mst. 5-10.
Kama hakuna toba watu hawa wanapaswa kujiandaa kukutana na Mungu wao (Linganisha Amosi 4:12).

(a) Hata ingawa Mungu amejaa na upendo, huruma, hatakubali kudhihakiwa. Tunapaswa kupata somo hili hata sisi siku hizi.

(b). Mashujaa wakuu wa mataifa waliakilishwa Kama Simba. (2Sam. 23).

(c). Watu hawajamrudia Yehova. Kwa hiyo Yehova haja badilisha hasira yake.

(d). Hawa watu walikuwa wamepotoshwa na Viongozi wao, waliokuwa wakiwadanganya kwamba ahadi za Mungu ni za lazima wala hazina Masharti.

Mst.17, 18. Mungu anaunganisha hali yao ya ndani (ya kiroho) na hali ya nje ya kuvamiwa na Babeli.

Nguvu za utawala wa Mungu kwa mataifa haufanywi kwa kutumia nguvu zake kama Mungu. Hutekelezwa kupitia watu wa kihistoria na wakala. Kwa sasa Babeli ndiye atakayetumika kama wakala wa kuadhibu Yuda.

Mst.19. Ufahamu wa Yeremia kuwa Yuda itakwenda utumwani unampa uchungu kama mama mwenye utungu wa kuzaa. Maangamizi juu ya maangamizi- huu ndiyo ujumbe wa Mungu; unapaswa kuzungumzwa, lakini Yeremia hawezi kuutangaza akiwa na utulivu. Yeye mjumbe wa Mungu lakini yeye pia ni sehemu ya watu. Hana la kufanya isipokuwa kujitambulisha kama mmoja wa kupata maafa. Haiwezikani kwake kuwa na amani huku watu wake wakienda kuangamia. (Linganisha na 8:18,19)

Mst. 22. Wapumbavu = hawafahamu, hawana maarifa. (Hosea 4:6). Watu watajibu nini? –Wamepotezwa na Kujisikia kwamba wako sahihi na Mungu. Ufahamu walio kuwa nao ni kutenda dhambi mbele za Mungu.

Mst.23-26. Ni sawa na mkanda unaotazamwa ukirudi nyuma. Kila kitu kilikuwa kikiviringishwa kurudi nyuma katika siku za muumbo, nuru kungeaka giza na uhai Kutoweka. Hii inaonyesha kuangamizwa kwa nje. Watu Wenjewe ndiyo walio sababisha hii.

Mst. 30. Usijisumbue.

## SURA YA TANO.

1. Mji umepotoka hakuna hata mmoja mwenye haki wa kufanya Yerusalemu ikombolewe (Mwa.18:23-33) Abrahamu / Sodoma 50-45,-40,--30,20,-10.
   - (a)wamepigwa
   - (b)wameangamizwa
   - (c)wamefanywa mioyo migumu.

Mst. 4. "maskini"haina maana watu ambao hawana kipato.Mtu wa kawaida Asiyejisikia kuwa na dini . Ni watu wazuri endapo wataongozwa vizuri

Mst.6. Ishi kama mnyama kufa kama mnyama.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Simba | - | Zephania 3:1-3 | - | Mkali |
| Mbwamwitu | - | Hab 1:6-8 | - | Mraruaji |
| Chui | - | Hosea 13:7 | - | Mwenye hila |

Mst 7-9. **Nitawasameheje?**

(a).Wamemwacha Yehova …………………...Mst7

(b) Wanawapakwa mifugo na mawe un7

(c) Ustawi wao umegeuka kuwa najisi un7

(d) Wazinzi …………………………………..7-8

(e) Yehova lazima alipize kizasi V9.

(Linganisha na mst. 29)

Mungu anataka kuwasamehe lakini kufanya hivyo bila wao kuonyesha toba, ni kumfanya Mungu kuonekana kama anayewaomba hali yao na yeye kuonekana asiye na msaada. Tatizo ni kwamba wamekwenda kupita mahali pa kurudi na kwa hiyo ni vigumu kwao kutubu. Israeli sasa wamesimama chini ya hukumu ya Yehova.

Nani, Nini, na jinsi gani, watu wanavyo abudu hawafanya akili zao kuwa bila thamani katika maisha.

Je! Mahubiri ya Yeremia yamekuwa ya kurudia rudia? Kama ujumbe unastahili kuhubiriwa unafaa kurudiwa tena. Inawezekana watu wasikumbuke hotuba yako, lakini baadaye watakumbuka ujumbe unaojaribu kuwafikishia.

12. Angalia nadharia hii kuhusu Mungu. Tunamweka akilini mwetu, nje pembeni mwa dunia tunakomtarajia kukaa na kututazama bila kujali ni nini tunachokifanya wala kutuadhibu pale tunapokosa.

Mst 21-23.

(a). Hawaoni …………………………………………………mst.21

(b). Hawasikii ……………..……………………………………mst.21

(c). Hawaniogopi …………………………………………….. ms.22

(d). Kwa hiyo hawako karibu nami…………………………… mst.23

Yehova anawaonyesha na pia anatuonyesha kwamba amekwisha weka mipaka kwa ajili ya wale watakaomtii katika sika zifaazo. Kama ni hivyo Kwa mini sisi wanadamu tunaasi mipaka aliyotuwekea?

Mts. 30-31.

| | | |
|---|---|---|
| Lakuchukiza | = | La ajabu. |
| Manabii | = | wa uongo |
| Makuhani | = | wanaofuata manabii wa uongo. |
| Watu | = | wanawafuata wote wawili na kwa hiyo wamepotea |

Yeremia ameshangazwa na manabii wa uongo pamoja na mafundisho yao na makuhani wanaokubaliana nao katika uovu wao. Sio hiyo tu, bali watu wanahitaji tu kile wanachokihitaji. Dini isiyodai chochote kutoka kwao.

Watu wanahitaji kutabua ni nini kinachowajia na kwa nini. Pia wanahitaji kutumainia siku za usoni. Sawa na jinsi msalaba wa Kristo utakapokuwa bila maana tusipoweka mbele tumaini tulilonalo katika ufufuo.

MARUDIO

Kazi ya kudondoa: 1:10; 7:11

1:5 Mungu alifamu kwamba Yeremia angelikuwa mtu wake hata kabla ya kuzaliwa.

1:17-19 Unafanya upande wako naye Mungu atafanya upande wake.

1:16 Muhtasari wa kitabu cha Yeremia

2:11 Hata mataifa hawabadilishi miungu yao.

4:27 Daima Mungu hushikilia mwanga wa tumaini

5:1 Hakuna hata mwenye haki hata mmoja wakutetea Yerusalemu

5:6 Ishi kama mnyama, kufa kama mnyama.

**SURA YA 6.**

Mst. 3. Jeshi la wavamiaji litakuwa sawa na wachungaji.

(a). Watamjilia

(b). Watapiga hema zao karibu naye.

(c). Watalisha kila mmoja mahali pake.

Mst. 4-5. Watakuwa na hamu ya kuharibu- watapenda kupigana usiku. Jambo ambalo halikuwa la kawaida katika siku za zamani.

Mst. 10-11. Mungu hakumtumainia Yeremia kuwa mhubiri mwenye Mafanikio(hata nasi) Anatutumainia kuwa waaminifu kwake na kutoa ujumbe wake tu.
Hatupendi kama na wao haukapenda kusikia kuhusu ghadhabu ya Mungu. Ulimweya wa dini unapenda watu wazugumzie upendo wa Mungu na kusahau ghadhaba yake. Wanafikiria kwanba upendo wa Mungu utafunika ghadhabu yake, Lakini hii ni kinyume na mafundisho yote ya Biblia.

Mst 14. Kilio cha uongo na ndugu wa uongo wakisema, amani, amani lakini kumbe hakuna amani.

Amani = Shalomu- hali kuwa na utulivu, mafanikio, bila maumivu.

Mst 16. Jibu: TAFUTA NJIA ZA ZAMANI " huu sio wito wa kurudia njia nzuri za zamani ,bali ni kurudia njia za asili alizoziweka Mungu.

Jibu la wanadamu: "hatutapita njia hizo".

Kwa sababu hakuna mtu anayesikia maonyo na kutoshirikiana na wenye dhambi, Hakuna atakaye epukana na kushiriki hukumu.

Mst. 20. Haijalishi ibada ni nzuri kwetu binafsi kiasi gani kwetu, maisha yetu yasipoenda sambamba na kile tunachokifanya katika ibada, tunayoyafanya yatakuwa machukizo kwa Mungu ‘’

Mst. 21. “Makwazo” = Kweli – kwa mwenye haki ni jiwe la msaada – kwa Mwenye dhambi ni makwazo.

Mst. 27-30. Fedha iliyo kataliwa. Yerusalemu imewekwa pa baya kwa hiyo haina Thamani kamili itakataliwa. Ni jambo la kushangaza kuona kwamba wayahudi wamekuwa watu wasio na msimamo wametoka kwa Yehova kwamba hawaoni kinachoendelea kati yao na kwao. Je ni tofauti na sisi leo hii?

**D. VITISHO VYA KWENDA UHAMISHO BABELI SURA 7-10.**

## SURA YA 7

## WITO KWA WAABUDU

**Maneno ya Yeremia yatachukuliwa kama usaliti. Hiyo ni matokeo ya dhana ya makuhani na wafalme. Dhana hii ilikuwa na madai kwanba kuwekwa imara kwa hekalu, na kulindwa kwake kulikuwa bila masharti.**

**Hii ilimpa Mungu mipaka katika utendaji wake na Israeli endapo walitenda dhambi. Katika maneno mengine, dhana hii ilikuwa ikimaanisha kwamba Israeli hawakuwa na haja ya kushikilia imani yao katika Yehova.**

Mst.2 Simana na kuhubiri malangoni mwa nyumba ya Bwana.

Mst.3 Kubakisha nchi haitatokana na haki yao ya urithi, sio kwa labda, sio kwa maandishi, isipokuwa tu, wakifanya haki na kutii.

Mst.8-20 Kulipwa ujira wao. Yuda amekataa tiba ya dhambi yao. Kwa hiyo ni lazima Yehovah aliharibu hekalu ili watu wapate kufahamu kwamba ukweli hauhubiriwi ndani yake. Ni dini ya uongo tu inayohusishwa pale. Kwa hiyo Hekalu nilazima liondoke.

Mst.10. Maneno ya uongo hayawezi kufaidi.

Mst.11. Ibada ni shughuli kama kawaida. Waasi wa sheria ya Mungu hao wanajaribu kuficha dhambi zao katika utakatifu wa huduma ya Ibada. Ibada yao sahihi imekawa kame vazi la nje tu la kufunika maisha yao ya uovu wanaoishi. Hii ni kujidanganya ilio waelekeza Israeli katika maangeamizi: Ni vipi umadhehebu siku hizi? Ni vipi kuhusu makanisa ya Bwana yaliyo mengi siku

hizi. (Mt 21:13)- " pango la wanyanganyi."

Mst.12. Walikuwa na wakati mgumu kwa sababu ya dhana yao kuhusu hekalu, katika kuamini kwamba Yerusalemu itatendewa na Yehova jinsi alivyo tendea Shilo.

Mst.15. Watu hawapendi desturi zao walizozizoea kushukiwa hasa zikihusiana na Dini. Kuna vitu viwili vya kuchunguza kuhusu hotuba hii,

(1) Mengi Yeremia anayoyasema hapa si mageni.

(2) Imani hutegemea ahadi ya mungu,lakini hatupaswi kubadili ahadi hizi kuwa bila masharti.Ibada na imani inapoonekana kuwa imekosa maana kwetu ni jambo la busara kwanza kutazama kwa karibu maisha tunayoishi sisi wenyewe kama yanafanana na neno la Mungu.

Mst.16. Kuna wakati sala haziwezi kusaidia .
Yeremia anawaambiwa usiwaombee linganisha na 11:14,14:11,1Yohana 5:16.

Mst.18. "Malikia wa mbinguni" wanawake walivutiwa sana katika ibada yao kwa Sababu iliwatamanisha silika nyingi ya kimsingi kama, ngono,uzazi,na kutabiri mambo yajayo (Elimu ya nyota).

Mst.20. Hasira ya Bwana itawaka na haitazima.

21-28. Katika amri kumi zenyewe hazidai sadaka dhabihu za kuteketezwa. Hii ilikuwa Muhimu sana kwa waisraeli, lakini pointi ni kwamba haikuwa ya lazima kwa imani ya watu (hasa wakiwa uhamishoni).

23. Tiini sauti yangu nami nitakuwa Mungu wenu.

28. Lakini usipotii ukweli ni kuagamia, kwa hiyo:

(a) Machinjo …………………..mst. 32
(b) Aibu…………………………mst 33
(c) Huzuni na mateso…………… mst 34

Kusikiliza neno la Mungu ni kuwa tayari kuongozwa maishani mwako na neno hilo. Hii ndiyo maana ya kusikiliza kunaomweleza mtu kutoa maisha yako ya dhambi kwa kutekeleza mambo ya dini. Kinyume cha aina hii ya kusikiliza, ni ya mtu binafsi inayohusu wewe , jamii, au serikali. Kunza kudai kuwa ndiye mwenye mamlaka.

## SURA YA 8

**Akili inayoelekeza katika mangamizi!**

Mst.3. Hii haipendezi kusoma. Yehova na Yeremia hawakuwaruhusu kujidanganya. Uongo ulitakiwa kuwekwa wazi na kuangamizwa. Fikira zao kwamba wanao usalama ulitakiwa pia kuangamizwa hapo ndipo kungelikuwako na tumaini la kweli.

Mst. 5-9

5. Kurudi nyuma mara kwa mara.

7. Hata ndege wanafahamu ni lini kuingia na kuondoka. Wanaishi maisha jinsi Mungu alivyo wapangia kuishi, Lakini Yuda hawawezi kuishi maisha waliopangiwa kuishi na Yehova. Inaonekana kana kwamba vitu vya asili vina akili kuliko mwanadamu.

8-9. Hekima gani iliomo ndani ya wenye hekima ?
kwetu sisi leo?

10-13. Watu hawa walikuwa wamepofuka kiasi kwamba hawakuweza kuona udanganyifu wa makuhani na wafalme. Hawakuweza kuona tofauti kati ya madai, ya kujiweka tayari na ukweli wenyewe. Angalia kwetu leo hii na uangalie historia ilivyo, angalia hatujabadilika hatuna tofauti na watu wa siku zile.

Mst.15. Matokeo ya hekima, makosa.

17. Zingatia tofauti hii kutoka kwa farasi na kufanyika nyoka.

20. Kwa hiyo hatuna usalama!

22. Hakuna (tiba) zeri katika Gileadi? Hakuna tiba kwa sababu ugonjwa una kina kirefu. Ibada ya sanamu imekithiri. Yuda wamekataa dawa iliopo. Tena picha inatofautiana wakati huu kutoka vitisho vya hofu kwenda kwa magonjwa, na huzuni.

## SURA YA 9:

## UPUMBAVU WA WATU

Mst. 1. Wote tumelia, lakini tukalia tena! Yeremia hana nia ile ya kusema, “mimi Siniliwaambia” bali yeye anasikia uchungu kwa ajili ya watu na kumwaga machozi yenye huzuni.

Mst.2.- Mithali 6:16-19.

Mst.4-6 Jamii pamoja na watu wengine hawawezi kuendelea kufanya vema kama watu wake wana lugha ya uongo.Hii inaonekana siku hizi kataka uchumi;

dani na maisha ya siasa. Tutajibu kwa Yehova kila tunacho kisema (Mathayo 12:36).

Mst.6. Kukataa kumjua Yehova!
Vipi? Hadaa!!
Matendo sahihi katika Ibada - Moyo mbovu?
Upendo sahihi wamafundisho -Upendo makosa kwa waliopotea?
Nia sahihi katika utoaji -Kuwajali ndugu kwa njia makosa.

Mst.9. Ikiwa watu wa Mungu watafahamu utakatifu wa Mungu kungekuwa na watu wengi wenye haki ulimwenguni.

Mst.14. Ukaidi na kuabudu sanamu ni sawa. Yote mawili yanaelekeza katika maangamizi ya kiroho.

Mst17-19. Kuhuzunika kwa ajili ya dhambi kwa hitaji. Inaonekona kwamba mtaalama wa uluzumi alihitajika kuwaongoza watu katika toba Pia ni kwamba watakaokufa watakawa wengi muno kiasi kwamba wataalamu wakulia hawatatoshe.

Mst.23-24. Usijisifu katika:

(a). Hekima
(b). Nguvu
(c). Utajiri

Bali tujisifu katika:-

(a). Ufahamu na
(b). Kumjua Yehova

Kwa kuwa Yehova anafanya:-

(a). Upendo wenye huruma
(b). Hukumu na
(c). Haki.
Linganisha 1.Kor.1.18-31

Wazo la “hekima” katika mazingira haya ni hekima ya kidunia. Sio wale walio na hekima machoni Mwa Mungu.

Mst.26. Mungu anasema hakuna tafauti kati ya waliotahiriwa na wasiotahiriwa kukiwa Hakuna imani na itii. Rumi 2:28;29

Zingatia: Kumbukumbu 10:16-17 tohara ya moyo inafuata mara na kuonyesha kwamba Mungu hana upendeleo wala yeye hachukuwi Rushwa.

Hii maana yake ni kwamba tohara ilikuwa ni alama ya utii wa Agano, wala haukuwapatia Israeli upendeleo. Kutofuatwa kwa tohara jinsi Paulo alivyokuwa akisema, kulikuja pale amri ya kutii isipofuatwa au isipotekelezwa. Kutofuata amri kwa Israeli kumekataliwa na Yeremia hata na Paulo naye.

## SURA 10

Mungu dhidi ya miungu.

Fungu la maandiko hili lina mawazo mawili yaliyosukuwa kwa pamoja.
(1) Kudhihaki ibada ya miungu miingine. (2-5,8,9,14,15) na
(2) Kusherekea maajabu na nguvu za Yehova, Mungu wa kweli na wa pekee (6,712,13,16).

Watu wametengenza miungu mingi sana kwa mfano uasili, (naturalism), tekinolojia, sayansi, utaifa au uzalendo, kiulaji (consumerism), na kiujeshi (militarism). Jambo muhimu ni kwamba vitu hivi vimeumbwa, na tunaviabadu badala ya kuabudu yeye aliye tuumba.

Mst2. Usijifunze njia za watu wasio mjua Bwana.

(a) Kidini
(b) Kitabia
1. Kama mtu Binafsi
2. Katika Biashara

Mst.5 Usiheshimu Uovu!
Miungu: Isio
(a) Sema
(b) Kwenda
(c) Fanya maovu au
(d) Fanya mema.

Mst.10 Heshimuni Yehova!
Yehova ni:
(a) Mungu wa kweli
(b) Mungu aliye Hai
(c) Mfalme wa Milele
(d) Mwenye ghadhabu

Mst.16 Fungu la maandiko "Sehemu ya Yakobo" na "Israeli" ni kabila la urithi wake Imegeuzwa kumaanisha Mungu atubariki"
"Mungu anahusiana nasi" hii ni kinyume na kusema "sisi ni wa Mungu".
Kama usemi wa kwanza ungeli kuwa kweli Ingelimaanisha tuna mmilki Mungu na tunaueza Kumtumia tupendavyo. Ya pili ina maana ya kwamba tunapaswa kujitoa kwa Yehova na kazi zake katika kila maisha yetu ya hadharani na nyumbani na hata ya Ibada.

Mst.23. Mungu hutia alama jiani! LAKINI mwanadamu hutafuta vinjia vya pembeni.

Mst.24. Kusahilisha- pamoja na haki = masahihisho.
Ku salihihsha – na uchungu = adhabu.
Tusiposikiliza masahihisho = Ghadhabu ya Mungu inakuja.

Tupende au tusipende Mungu ataweza kutupatia nidhamu. Kwa hiyo tuwe na uhakika kwamba atafanya kwa njia ya haki sio kama mtu asiyejali.
Hii inatueleza kwamba hata katika shida tunapaswa kumtumania Mungu na kuomba majaliwa yake kwa ajili ya wema wetu. (Rumi 8:28).

MARUDIO

Mstari wa kukariri Yeremia 1:10,7:11,13:23.

1:17-19 Unafanya upande wako na Mungu atafanya upande wake.
2:11 Hata mataifa hawabadihishi Mungu wao.
4:27 Mungu daima hushikilia mwanga wa tumaini.
5:6 Ishi sawa na mnyama, kufa kama mnyama.
7:16 Kuna pointi maombi hayawezi kusaidia.
9:9 Kama watu Mungu wangeli fahamu utakatifu wa Mungu, kungelikuwa na wenye kaki wengi Ulimaenguni.
10:5 Muingu hawezi kukudhuru.Wala hawawezi kukutendea mema.
10:24 Tusiposikiliza masahihisho, ghadhabu inakuja.

E. AGANO LILILOVUNJIKA NA ISHARA YA MKANDA.

SURA 11.

Kutotii kwa Yuda na matokeo yake

Mst.1. Yuda ilikuwa imeshindwa katika maisha yake ya dini; lakini adhabu yake ilikuja Katika maisha yake ya kila siku na ya kisiasa.

Mst.2. “Sikiliza maneno” ni yatakiwayo, sio kuyasikiliza tu bali ni yatakiwayo,ya kuyatii.

Mst3-5. Sheria iliposomwa kwa wana wa Israeli; wangeliitikia “Amina” (naiwe hivyo) wakati wowote laana ilipokuwa ikusomwa, Yeremia alifikia (na iwe hivyo)

Mst.11. Laana ni juu yao. Ingelikuwa heri kama wasingelifanyika watu wa Mungu, kuliko kufanyika na baadaye kuanguka.

Ni sawa hata leo na sisi wakristo (Lingamisha Lk12:48; Waebramia 10:24-31).

Mst.11-13 Sala za wasiomcha Mungu hazisikilizwi

Mungu kwa kila mji.

Leo? Vipi? Kila mji unaonekana kuwa na dhambi ya aina yake.
Mst.14. USIWAOMBEE!! (Linganisha 7:16,14:11,1Yohana 5:16)
Mst.18-23 Anathothi – Watu wa kwao na Yeremia wana fanya, njama za kumua.

Mst.19. Sawa na kando wakufungwa aliyezoea mazingira ya nyumbani akitolewa nje ya boma hawezi kuwa na habari kama inapelekwa kuchinjwa.

Mst.23. HAKUNA MABAKII

**SURA 12**

Ushahidi zaidi juu ya Yuda.

Mst.1-6 Waovu huwa na mafanikio:
(a). Mali ya dunia – Ndiyo
(b). Mali ya kiroho – Hapana.

Viumbe vyote huteseka kwa sababu ya dhambi.-- (Rumi 8:18-22, Waebrania 2:9

Mst5,6 Yeremia alikuwa ameuliz "kwa nini? Lakini daima Mungu hajibu vizuri, kiundani. Jibu lake ndilo hili "Unakiri kwamba Hali ni mbaya sana, Mabaya zaidi ya kuja!"
Mst.7. Linganisha namna ya kuachwa huku na kule kwa Yesu katika (Mathayo 27:46)
. Mst7-17 Lakika hukumu inakuja (Soma Zaburi 5:5, linganisha. Kumbu.25:13-16,Zaburi 11:5).

11. Hawa wavamizi hawaingihii utawala wa Mungu bali ni chombo Mungu anachokitumia kutekeleza utawala wake, Yehova anahuzunika kwa sababu hawa wavamiaji ni chombo chake cha kutekeleza hasiri yake na haki.

Mst 13 Walikuwa wamedanganywa hawakujua kwamba dhana yao kwamba Yehova hawezi kuliacha Hekalu na Yerusalemu kwa sababu ya dhambi zao ingelimletea Yehova kughadhabika na hata kujiondoa. Ukweli ni kwamba ilikuwa ni kinyume chake. Hata na sisi leo hii tunapaswa kuwa wangalifu namna tunavyo litumia neno la Mungu.

Mst 16,17. Ikiwa-ndipo (mara mbili) Mistari hii inaonyesha kwamba Yehova hana upendeleo kwa mataifa. Mataifa yote yanapaswa kutii neno lake na kuwajibika sawa sawa na Israeli.

**SURA 13**

KIBURI- Ndilo tatizo la Yuda.

Mst 1-11 Mshipi au mkanda wa kitani
(a) Mwanzoni safi na maalum. ……………………….. Mst 1
(b) Baadaye mchafu na haufai……………………… Mst 7

(c) Kiburi kuangamizwa…………………………………Mst 9

Yuda ni sawa na mshipi ambao ulikuwa mzuri na sasa haufai kwa chochote.

Mst 10,11 Matokeo ya kutomtii Yehova.

Hatimsho ya 1-11 :

| Amri | Fafanusi |
|---|---|
| Nunua na kuvaa. Mst.1,2 | Jishikilia kwa Yehova. (Mst 11) |
| Ondoa na kuficha. Mst. 3-5 | Israeli wanamkataa Yehova(Mst.10) |
| Utwae na kuona ubovu wake.Mst.6,7 | Israeli hawafai (mst. 9) |

Mst 16. "Giza" limetafsiriwa kivuli cha mauti katika Zab. 23:4. Inaweza pia kutafsiriwa kifo katika, au giza nene.

Mst 18,19 Yehova anatangaza kwamba madai ya kuwa sisi ni wa ukoo wa ufalme yametenguliwa. Madai haya yameondolewa kwa sababu ya kukosa imani na utii. Na hii yote ni kwa sababu ya kutomsikili za Yehova.

Mst 22. Kwa nini mwadhibiwe? DHAMBI!

Mst 23. Umewekwa katika hali yako (Mkushi na chui).
Agano la kale halijui fundisho la dhambi ya asili. Habari ya Bustani ya Edeni haikutafsiriwa hivyo katika Agano la kale. Au na Wayahudi na wasomi wa badai.

Mst 27. Ee Yerusalemu utakuja kuwasafi? Inaonekana kwamba Yerusalemu ilifanana Sawa na nzoga. Mzogo ni kitu najisi na hakifai kwa Israeli Kuishi ndani. Bila shaka hata hakifai hata kwa Yehova kuishi ndani.

F. UKAME ISHIRA YA NABII ASIYE OA, ONYO KUHUSU SABATO SURA 14-17.

SURA 14

NJAA KUU.

1-6. Maelezo kuhusu njaa…. ……………………………………………..linganisha 2,4

7-9. Majibu ya Yermia:

(a) Dhambi zetu hutushuhudia.

(b) Tuadhibu kwa ajili ya jina lako

(c) Kurudi kwetu nyuma kumekuwa kwingi.

(d) Dhambi zetu nijuu ya Yehova.

Katika hali yake ya Mwisho, ni sala inayohitaji uwepo wa Yehova.Yehova amatao jibu lake Mst.11,12

Mst.11,12 Usiwaombee
Sitawakubali
Nitawaadhibu
(a) Kwa upanga
(b) Kwa njaa
(c) Kwa tauni

Mst 13-16 Manabili wa uongo husema:
(a) Hakuna upanga
(b) Hakuna njaa
(c) Bali kuna amani (Kumbu.18:20-22 13:1-15)

Mst.15 Manabili wa Uongo walidanganywa au walijidanganya. Ni mara ngapi watu wanatoa maamuzi na kufudisha mafundisho ya uongo? Kwa siku za leo wanaozidi sana kutoa mafundisho ya uongo ni wale wanaodai kuwa wanaongozwa na Roho Mtakatifu. Lakini kosa ni kosa na ni dhambi.

TOBA

Mst.17-22

Manabii wa uongo wenu husema amani…………….……Hakuna amani.
Manabii wa uongo wenu- wakati wa kuponywa…….……….Kuna shida

Chanzo cha matatizo yao ni uongozi ulioshindwa kuwajibika. Katika kushindwa huku hawana ufahamu wa Mungu, kwa hiyo hawatamani kumtil. Isaeli hata na sisi tunandelea kutomtii Bwana na kutarajia mambo kuwa safi na Mungu. Kusikiliza neno la Mungu kwa wangalifu na toba ya kweli hutakiwa.

SURA 15

Yuda wameenda mbali: Hata Musa na Samweli hawawezi kubadilisha mawazo ya Yehova:

Mst.1 Ondoa Yuda machoni pangu.

Musa na Samweli walijulika kwa sababu ya maombi yao ya bidii.
Haya ni maneno makali sana ya kuwataakaa.

2-9 Adhabu yao itakamilika.

- Watavuna walicho kuwa wakipanda.
(Linganisha Galatia 6:8, ufunuo 14:9b,10)

Mst 4. Kwa sababu ya Manase. (Lingasha 2 Nyakali 33)
Alifanyia Yuda kile Ahabu alichokifanyia Israeli.

Mst5-9 Mungu anatumia picha ya kundi kubwa la wa mama wanye huzuni kuwaonyesha jinsi gani huzuni ya Yuda itakavyokuwa. Watoto saba walichukuliwa kuwa familia kamili na kwa hiyo ni kuonyesha kwamba familia hiyo imefutwa duniani.

Mst 6 Yehova amechoshwa na Yuda.

Mst 15-19 Yeremia amechoshwa pia na Yuda.
Je kuna akina Yeremia kati yetu?
Yeremia amekuwa mwaminifu kwa Yehova na kwa hiyo ombi hili ni kutokana na kile anachostahili kupata kama mtumishi mtiifu.

Mst 20-21 Jipe moyo, Yeremia-Yehova amrudia ahadi yake aliyoitoa katika sura ya kwanza.

MARUDIO

1:17-19 Unafanya upande wako na Mungu atafanya upande wake.
2:11 Hata mataifa hawabadihishi Mungu wao.
4:27 Mungu daima hushikilia mwanga wa tumaini.
5:6 Ishi sawa na mnyama, kufa kama mnyama.
7:16 Kuna pointi maombi hayawezi kusaidia.
9:9 Kama watu Mungu wangeli fahamu utakatifu wa Mungu, kungelikuwa na wenye kaki wengi Ulimaenguni.
10:5 Muingu hawezi kukudhuru.Wala hawawezi kukutendea mema.
10:24 Tusiposikiliza masahihisho, ghadhabu inakuja.
11:11-13 Maombi ya wasio haki haisikilizwi.

SURA 16.

ADHABU NA MAANGAMIZI KUWA KAMILI
!
Mst.1-4 <u>Yehova anamwambia Yeremia:</u>
(a) Usioe!
(b) Usipate watoto
(c) Adhabu itakuwa kali.

Kuishi bila kuoa halikuwa chaguo la mtu katika Israeli. Ndoa yake ilipangwa na wazazi kwa kudumisha jina la familia na namna ya pato. Kwa hiyo bila mke lilikuwa kinyume cha maisha ya kila siku;ingelimfanya Yeremia kuonekana mtu asiye wa kawaida katika jamii. Watu wangelimshuku na ujumbe wake usingeli pendwa.

Mst.5 . Usiingie katika huzuni na watu.

Nimekwisha ondoa:
(a) Amani
(b) Upendo wenye huruma
(c) Rehema

Yeremia alikuwa akiishi maisha mfano wa kutazamwa.maisha yake yangekuwa Mfano wa mchafuko wa familia na maisha ya jamii kama ilivyo kuwa imejulikana na watu hawa.

Mst 9. Furaha yote katika nchi itakoma. Hakutakuwa hata na ndoa.

Mst.13. Ni nani anayeweza kupona bila upendeleo wa Mungu?

Mst.14. Mungu amekufa! (maangmivu ni kamilifu)

Mst.15. Hapana (Mabaki)

Safari ya kuondoka Misri ilikuwa tukio ambalo Israeli waligipima maisha yao nayo na kutafsiri uzoefu wao katika historia.Yehova anasema watakwenda kupata pointi mpya ya marejeo na hiyo itakuwa kurudi kwao kutoka uhamishoni.

**SURA 17**

Mst .1 Dhambi zako ziko wazi (Linganisha Ayubu 19:23-25)

Mst.5 Usiweke tumaini lako katika wanadamu.

Mst.7 Mtumaini Mungu badala ya mwanadamu.

Mst.8 Linganisha (Zaburi1)

Mst.9-11 Fanya uovu –Vuna uovu.

Mst 11. Kware alijulikana kwa kukusanya mayayi ambayo siya kwake. Wazo ni kwamba jinsi kware walivyo,wale waliojikusanyia kimakosa kutoka watu wengine hawatavifuria .

Mst.14 Mungu peke ndiye wokovu.

Mst 15. (Linganisha 2Petro 3:4)

Mst 27. Ikiwa-Ndipo.
Hekalu Halikuhutajika kutunza Sabato. Watu hawakutakiwa kwenda Hekaluni siku ya Sabato ndipo waweze kuabudu katika siku hiyo. Wangeliweza

kutunza sabato mahali popote duniani. Wangelijifunza sheria na kutii maagizo yake popte walikoishi hata wakiwa uhamishoni.

G. ISHARA YA MFINYANZI…..SURA 18-20

**SURA 18.**

Haki ya mfinyanzi:-

1-9 Mfinyanzi

Kurudia kukitengeneza chombo ambacho hakikufaa.

Mst 1-6.Ikiwa mfinyanzi hapendezwi na sura ya chombo anacho kitengeneza anaweza kukibonda na kutengeneza anavyoona kuwa kitafaa kwa matumizi yake.
Walakini udongo huo hautafaa kwa matumizi ya badaaye.
Mfano huu unahusu Yehova na Israeli Yuda.

Mst.9-10.Ahadi za Mungu zote ni zenye masharti!
Yona – Ninawi.

Mst. 12. hakuna matumaini………………………Kujaribu kutuongoa.

Mst 13-17 Kwa hiyo Yehova anageuka na kuwaacha.
Ukiondoa theluji kutoka Lebanoni itabadilika kuwa maji na kukoma kuwa theluji. Ikiwa Israeli inajiondoa kwa Yehova,Itakoma kuwa Israeli.

Mst 18. kukabiliana na yule anayeleta tofauti au ujumbe wasio ukubali ni jambo la kawaida kwa wale waliomo katika uongozi wa siasa au wa dini.

Kupanga "mipango/njama," inaonyesha kwamba hu ni upinzani ulio tengenezwa kumpinga Yeremia. Ni upinzani wakutisha, na ni mpango uliokusudiwa kunyamazisha mtu "mhaini."

23. Mungu hamsamehi bila kutubu kwanza.

**SURA 19**

**CHOMBO KILICHO VUNJIKA. KUANGAMIZWA KWA CHOMBO KINACHOONEKANA KUWA HAKIFAI!**

Mst.1,2. Neno la Mungu silakushikiliwa sirini bali ni la kuongelewa katikati ya watu.

Mst3 Hata habari ya adhabu yako itakusabishia hofu na mshangao.

Mst 7-9 Zingatia Yehova anasema, "nita" mara tano katika misitari hii. Hakuna Wakala wa Mungu hata mmoja katika anayetajwa; Mungu anawajibika moja kwa moja katika vitendo hivi.

Mst.9. Hii ni sababu nzuri ya Yeremia kutokuoa.

Mst.10-11.Knvunja gudulia na taifa.

Mst.15. Maangamizi haya sio kwa kuwadhibu watu, kwa sababu hakukuwa na wito wakuwataka kutubu.Yuda wamefika mbali.hakuna kuponyoka.hukumu hii ni ya mwisho, kubwa tena, dhahiri, isiohitaji mdaholo au majadiliano.

**SURA 20**

**Majaribu ya Yeremia na Maombolezo.**

Mst.1. Sala hii inaonyesha udhaifu pamoja na nguvu.
Udhaifu katika Yeremia,lakini nguvu katika Yehova aliye na uwezo wa kufanya kila anacha kipanga.

Mst 4. Je! Tunaweza kuwa hofu kwetu wenyewa na kwa watu wengine?

Mst 7. (Linganisho 1 Wafalme 22:8).

Mst9. Nitaondoka! au Nitaacha!

Mst10. Ni nani anayekutazama?

Mst 14-18. Kuchukiwa kwa ajili ya Yehova (linganisha Ayubu 3:1-19)

Biblia mara kwa mara ina haki. Yehova hatufichi kwamba kulipokea neno lake Wakati mwingine inaweza kuwa na gharama kwetu. Imani yenye kina kama ya Yeremia haiwezi kutuelekeza katika maisha laini na yenye usalama, bali ni Katika matatizo. Wakati mwingine ni kutoka matatizo hadi matatizo.

**MARUDIO**

**Mstari wa kukariri Yeremia 1:10,7:11,13:23,17:5, 20:9,23:29**

1:17-19 Unafanya upande wako na Mungu atafanya upande wake.
2:11 Hata mataifa hawabadihishi Mungu wao.
4:27 Mungu daima hushikilia mwanga wa tumaini.
5:6 Ishi sawa na mnyama, kufa kama mnyama.
7:16 Kuna pointi maombi hayawezi kusaidia.
9:9 Kama watu Mungu wangeli fahamu utakatifu wa Mungu, kungelikuwa na wenye kaki wengi Ulimaenguni.
10:5 Muingu hawezi kukudhuru.Wala hawawezi kukutendea mema.
10:24 Tusiposikiliza masahihisho, ghadhabu inakuja.
11:11-13 Maombi ya wasiomcha Mungu hayasikilizwi

14:7 Dhambi zetu zinatushuhudia
18:8-10 Ahadi za Mungu zote ni zenye masharti.
20:4 Tunaweza kuwa hofu kwetu wenyewe na kwa marafiki zetu.

UNABII WA BAADAYE YEHOVA KIM NA ZAKARIA(SURA 21-39)

A. NEBUKADEREZA FIMBO YA MUNGU YA KUMWADHIBU SEDIKIA NA YERUSALEMU……………………SURA 21-29.

**SURA 21.**

MST.1,2. Sedekia ni sawa na mtu anayeendelea kwenda kwa daktari na maradhi, lakini hayuko tayari kuchukuwa ushauri wa daktari au madawa ya kumponya anayopewa.

Nia ya Sedikia inaonekana kama kusema,"haiwezi kutendeka kwetu" "Nia kama hii daima ni hatari, hasa zaidi ikiwa inadaiwa kutokana na imani,za kidini zinazoshikiliwa kwa kina. Viongozi wa Yeremia wamempinga Yeremia tangu mwanzo, lakini sasa wanalazimishwa kuja kwa Yeremia kama jambo la mwisho. Mikakati yao na utaratibu wao umeshindwa na sasa , mwishowe neno la Mungu linapaswa kuchukuliwa kama kweli.

Mst 5. Yehova anawapigania watu wake kwa kupigana nao (linganisha 2Petro 2:20-21)

Mst8-10. Njia ya uzima na njia ya mauti

Mst11,12. Siasa, tabia,haki haviwezi kutenganishwa !Ikiwa Serikali inapuuzia haki na Tabia njema, moto wa Yehova una haki wa kuujia utawala huo.Tunaweza Tukajisikia kwamba unakuja taratibu, lakini Bwana peke yake ndiye anayejua kama Uovu wetu umejaa na ni wakati wake kuingilia kati. (linganisha na Mwanzo15:16)

Mst.14. Yehova ni mwenye haki.

**SURA 22.**

1-3 Usiseme tu –vitendo huvuma sana kuliko maneno
4,5 Angalia neno "Ikiwa"hii ni moja ya maneno muhimu au ya ufunguo wa ujumbe wa nabii. Kulikuwa na masharti ya kufua twa kwa mjukuu wa Daudi kukalia juu ya kiti cha enzi .Mfalme na kiti chake cha enzi viko chini ya Yehova.

Nafasi hiyo sio bila Masharti.

Mst.8 KWA NINI KUTENDA HIVI?

Mst.9 KWA SABABU YA DHAMBI!

Mst.11 Shallumu =Yehoiakimu (mst18)

Mst13.Nyumba iliyojengwa juu ya haki na biashara iliyojengwa juu ya haki.

Mst15-17 Tofauti yao na Daudi.

Mst.18,19 Sedekia ni wa kufa na mwili wake kutupwa, sawa na mnyama najisi nje Ya kuta za mji.

Mst20 Yuda hatapata msaada katika washirika wake wa kisiasa kwa sababu,nao pia Wamekwisha shindwa, kwanza hakukuwa na sababu ya Yuda kuwa na washirika Hao.Yehova alitakiwa kuwa mtetezi wao,sio silaha za mwili.
(linganisha na Hosea 8:9)

Mst.24 "Pete yenye muhuri".Ulikuwa wa kibinafsi. Kila moja ulitofautiana na mwingine.Ulitumika kuthibitisha uhalali kwa kuupigilia katika taa juu ya Maandishi. Yehova anasema kwamba ikiwa konia angekuwako kwake ,bado Angelibadua na kutupa mbali

Mst.30 Mungu hasemi kwamba Konia asingekuwa na watoto bali ni kwamba Hakuna mtoto wake atakayeketi katika kiti chake cha enzi cha Daudi katika Yerusalemu na kuendelea.
Hakutakuwa na mrithi wa Konia (juu ya kiti cha Daudi) Ahadi ya 2Sam7:13-16

Haikuwa masharti jinsi walivyodhania. Walikuwa ni watu wa kuchagua sehemu Za kuamini katika Biblia (zaburi132:11,12) inaonyesha wazi kwamba ufalme na Kiti cha enzi vilikuwa vyenye masharti kutegemea utii wao kwa Yehova. Kungelikuwa na mrithi kama sheria za Mungu wangelizitii.Bila utii hakuna Urithi hapa duniani

Mst.24-30 Wa kabla ya utawala wa miaka1000 (upremilliniamu)

(a)Ahadi ya mzao :
Yehoiayakini au Konia =Yekonia
(linganisha Yer22:24-30, Mathayo1:11,12

Kwa kufuata unabii huu, wanaodai kuwa Yesu atarudi na kutawala miaka elfu moja katika kiti cha Daudi kiti cha Konia ni waongo kwa sababu Yesu ni wa ukoo wa Konia

(b)Ahadi ya nchi –Kumbukumbu19:1-10(linganisha na Yoshua 20:7-8)

(c)Nyongeza Nehemia 9:8;Yoshua 21:43-45; 1Wafalme 4:21, 30:10,11

## SURA .23

**Hukumu bila tumaini itaangamiza roho na tumaini pasipo na hukumu Ni usemi wenye hekima tu.**

Mst1 Wachungaji walikuwa nani kipindi kile –nani sasa kuhusu wachungaji zaidi Angalia hapa Yesu alidai kuwa mchungaji mwema Yohana10:11

Mst3 Mabaki –kurudishwa

Mst4 Ezra, Nehemia n.k

Mst 5,6 Utabiri kuhusu Kristo (linganisha 2Sam.7:12-17)Bwana aliye haki yetu.

Mst7,8 Mungu anawaahidi kuwafanya upya, lakini itakuja tu baada na kwa njia ya kwenda uhamishoni

Mst9-40 Manabii wa uongo …….leo je?
(a)Mjaribu nabii wa kweli –(kumb18:20-22,13:1-5)
(b)Mathayo 24:11wengi huinuka na kudanganya

Kariri: Isaya 8:20 "Na waende kwa sheria na ushuhuda ikiwa hawasemi Sawasawa na neno hili,bila shaka kwa hao hapana asubuhi"

Mst9-10 Kama wazinzi …….walisababisha ukame

Mst11 Katika huduma ya hekaluni

Mst13 Ilisababisha kuanguka kwa Israeli

Mst14 Jambo baya katika Yerusalemu.Viongozi wa kidini walishikilia utaratibu Mwovu wa wafalme na washauri wao.Walifanya kuwa halali kwa kutoonyesha Uovu wao,na kwa hiyo walizaa uovu zaidi.
"uzinzi"unaenda pamoja na mfumo wa siasa uliopotoka unagusa kila sehemu ya maisha,kiuchumi na kisiasa

Mst17. Hakuna uovu

Mst21,22 Ni nani aliyewatuma?si Yehova
Manabii wa uongo hawawezi kwa uhalali kusema "Ndivyo asema Bwana" Mamlaka yao hayatoki kwa Yehova. Yanatoka ndani yao wenyewe mkuu wa

Mamlaka yao ni Shetani

Mst23,24 Mungu hayupo karibu na kupatikana kwao,Bali hatuwezi kumtoroka

Mst25 Moses Kolola-Mwakasege

Mst26-31 Manabii hao wangelisema ukweli (mst28)
Lakini uongo wao umefanya jina la Yehova limesahauliwa (mst27)Neno lake
Limechukuliwa bure (mst31)

Mst29 Neno langu ni sawa na moto …..na nyundo

Mst32-40 (mzigo) wa mausia : matamshi mazito
Kutumia mausia (mzigo )kwa njia ya dhihaka

Mst34 usitumie usemi huo

## SURA YA 24

**Mtini mzuri na mbaya**

Mst1. Kama Danieli 1:1uhamishoni( mateka)

Mst2 Hali ya tini

Mst5 Tini nzuri inawakilisha wale wa uhamishoni

Mst 8,9 Tini mbaya ni akina nani?wale wanaopinga

Mst10 Maangaamizi

## SURA YA 25

Mst.1 Mwaka wa nne wa Yehoyakimu

Mst3. Kwa muda gani? Unabii wa miaka ishirini na tatu

Mst4. Lakini hujasikiliza!

Mst4-10. Inaelezea tena unabii uliopita

Mst11. Mwisho wa utumwa wa Babeli ni miaka sabini (linganisha 29:10)

Mst12. “Milele”sio muda usio na kikomo,bali ni wakati ujao
-Yehova anatumia watu wengine kutekeleza adhabu yake
-Lakini wao nao hawaendi bila kuadhibiwa

Mst17,18 Mataifa yote yatakuwa chini ya hukumu lakini angalia kwamba hukumu hiyo Huanzia katika nyumba ya Mungu 1Petro4:17

Mst37. Nchi

**SURA 26.**

YEHOYAKIMU -TISHIO KWA YEREMIA

1. Kuanzia kabisa mwanzo wa utawala wa Yehoyakimu neno la Yehova Halikukaribishwa, lilitemwa na kupingwa na wale waliokuwa katika serikali Yake

Mst2. Katika uwanja wa Hekalu

Mst3. Kwa nini labda watatubu (mmoja moja.)

Mst7. Ni nani aliyesikia?

Mst9. Angalia walikasirika alipozungumza juu ya Yerusalemu.Walifikiria Yerusalemu haikuwezekana kukosolewa (linganisha Amosi7:12,13)

Mst11. Yeremia anastahili kufa! Kwa nini?

Makuhani na manabii wanataka apewe adhabu ya kifo kwa kile walichokuwa Wakikiona kama unabii wa uongo. Angalia walishikilia sana kuhusu unabii wa Kinyume na Yerusalemu – na kusahau wito wake wa kutaka watubu.
Hii ni kunukulu sehemu. Hii ni kunukulu nje ya mazingira ni silaha inayotumika sana katika madhehebu na wapizani wa ukweli.

Wale waliokuwa wakimpinga Yeremia walidhania kwamba wakimnyazisha neno la Mungu litakwwa limetanguliwa.

12,13. <u>Kujitetea kwa Yeremia kuna sehemu mbili:</u>
(a) <u>Haya si maneno yangu, ni</u>
(b) <u>maneno ya Yehova.</u>

i. <u>Maneno ya Mungu kwenu sio tishio.</u>
ii. <u>Ni nafasi kwenu ili mpate kutubu.</u>

14. Nifanyeni mtakalo.

15. LAKINI!

16. Huwezi ukafahamu ni nani atakaye kuja kwenu kuwatetea.

18. Mikaya Ni nini kilichotendeka? –Hezekia alitubu
Urija- Ni nini kilichotendeka kwake- Yehoyakimu alimua. (linga. Mika 3:12)

24. Lakini Ahikamu alimwokoa Yeremia- Linganha na 1:17-19
Yeremia ameokolewa kutoka katika majanga yake, lakini majanga yake mapya ni kupuuzwa na wale anao wahubiria. Ni jambo la kuzunisha ukifahamu kwamba nchi na watu walikuwa wakienda uhamishoni kwa sababu ya hiyo.

**SURA 27.**

Wale walio katika serekali au mamlaka wanakaribisha sana msaada ukitolewa na Kanisa na kuchukulia kama kitu cha kawaida kinacho wafaa. Lakini Kanisa linapoanza kukosoa waliomo mamlakani,wananza kusema kwamba Kanisa linaingilia mambo yosiyowahusu. Kwa nini msaada uwe halali na kukoselewa kusiwe halali?

Mst1-7. Mwanzo wa utawala Sedekia.

Mst 8. "Upanga, njaa,na tauni" matokeo ya kawaida yanayotokana na vita.

Mst12. Utawala wa sedekia

Mst12,13 Kwenda utumwami ni uzima na kupinga ni mauti!

Mst16,17. Angalia hapa somo ni kurudi kwa vyombo vya nyumba ya Bwana. Vyombo hivi vilinajisiwa kwa kuviondoa Hekalumi na kuvifanya kuwa kama mateka.

Mst18. Ikiwa manabii hawa wanaompinga Yeremia ni manabii wa kweli wafanye upatanisho wao na Yehova na kukomesha kupelekwa kawa vyombo vya Hekalu Babeli. Hapo ndipo watu watawaamini kuliko Yeremia.

Mst22. Vyombo havijapotea kutoka Hekalu ni milele. Isipokuwa vitakwenda kwa kipindi kirefu. Vitarudi Yehova atakapopenda tu, sio kabla.

Yehova kupitia Yeremia, anatangaza hali mbaya ya siku zijazo za Yerusalemu. Lakini Ukiangalia,hawajaachwa bila tumaini.

**SURA 28**.

**Yeremia dhidi ya Hanania**.

**<u>Utabiri wa Hanania</u>**.

<u>(a) Nira ya Babeli imevunjwa………mst4,10</u>

(b) Vyombo kurudi katika miaka miwili…..mst 3
(c) Mfalme Yekonia kurudi toka uhamishoni …….mst 4
(d) Mateka wote kurudi toka uhamishoni ……..6.

Jibu la Yeremia.

(a) Amina……….mst 6
Linganisha na 1Wafalme 22:13-18 jibu la dhihaka kwa Ahabu.

(b) Nira ya Babeli niya chuma, sio ya mti.

(c) Hata wanyawa wa kondeni watatii….mst 14

(d) Yehova haja kutuma ………mst15

(e) Unawafanya hawa watu kuamini Uongo mst.15

(f) Utakufa mwaka huu ……….mst 16

linganisha 2Thess. 2:10-12

VUMILIA! Linganisha. Yakobo 5:11,Mathayo 10:26

Hanania anajikuta kuwa ni vigumu sana kwake kumsikiza Yeremia akiendelea kumpinga mawzo yake ya kina mara kwa mara.

Mst.16 Hanania alitangazia Yuda uzima kwa hiyo Yehova alimtangazia mauti.
Hanania ni mwasi na kwa sababu ni mwasi,atapokea ghadhabu ya Mungu.

## SURA 29.

Mst.1-23 Barua ya Yeremia kwa wa uhamisho.

(a) Jengeni nyumba…………………………………….mst 5
(b) Pandeni mashamba………………………………… mst 5
(c) Oaeni wake ………………………………………mst 6
(d) Zaeni watoto……………………………………...mst 6
(e) Ombeeni amani katika miji yenu ………………….. mst 7
(f) Waozeni binti zenu…………………………………. mst 6
(g) Msiwasikilize manbii mlio nao…………………….. mst 8
(h) Ntarudi baada miaka 70……………………………..mst 10,11
(i) Mtanitafuta na kunipato ……………………………. mst 13
(j) Nitawaadhibu manabii wa uongo…………………… mst15-23

Angalia walitakiwa kuwaombea maadui zao (e).Kuwaombea heri,sio maovu.
Hii ni mpya. Linganisha na Mathayo 5:44.
Angalia pia watamkuta Yehova katika uhamisho wao (1). Wamepoteza yote waliofikiria kuwa muhimu katika imani yao. Hekalu, dhabihu, n.k . Lakini Yehova anasema atawasikiliza popote walipo ikiwa maisha yao yataonyesa imani na utii unaotokiwa na Yehova.
Hata wakiwa uhamishoni Yuda wataongezeka sawa sawa na walivyoongezeka walivyo kuwa kule Misri. Mungu angali anathibitisha na kwa hiyo Yuda inapaswa kujitayarisha kwa kurudi kwake.
“ Wala sivyo tu, ila mfurahi katika dhiki pia, mkijua ya kuwa dhiki kazi yake ni kuleta saburi, na kazi ya saburi ni uthabiti wa moyo na kazi ya uthabiti wa moyo ni tumaini. Na tumaini haitahayarishi…….” Rumi 5:3-5b.
Mst. 10 Mwisho wa utumwa Babeli utakuwa katika mwaka wa 70: linganisha na 25:11-12.

Jinsi uhamisho ulivyo hukumu ya kuwangamiza kwa Yuda, kurudi kwao ndilo tumaini lake kuu, tamaa ya Mungu na zawadi ya Yuda

Mst.20-23. Wale wanaopinga hukumu ya Yehova, au tumaimi analolitoa watafikishwa katika mwisho mbaya.

Mst.24-29 Jibu la wauhamisho: MWEKENI YEREMIA GEREZANI
Kuamini uongo kunaweza kuelekeza katika vitendo vibaya sana. Jambo La kuhuzunisha ni kwamba wanafanya matendo ya upumbavu katika jina La dini. (Kwangalia kwa haraka haraka historia ya kanisa la “kikristo” inathibitisha hii mara kwa mara.)

Mst 30-32 Manabii wa uongo walio wachochea kuandika wanakwenda kufa.
Kwakuangalia nyuma katika sura 26-29 tunaona mahubiri ya Yeremia karibu yamsababishia kuwua (.26) alijaribu kushawishi mkatano wa kimataifa (27) anabishana na manabii wa uongo (SURA28) anaandika barua inayo sadikiwa kuwa ya uhaini kwa wa uhamisho (SURA29) Mtu huyu alikuwa akitabiri na kufundisha ukweli bila kujali ni matokeo gani mabaya yangelitokea kwake.

**B. Ufalme wakimasili wa siku zijazo…………………….SURA 30-32**

## SURA 30

Dini itaeleza ulimwengu kidogo sana ikiwa inatoa maafa badala ya matumaini.

3. Mstari huu unaelezea kugeuka kwa uovu maishani Mwao na wakati watakapopata imani na utii,kuwa watu wake, hapo ndipo Yehova atakapowabariki na uzima mkamilifu.

10-11. Ni pamaja nawe,LAKINI nitakuadhibu.

13 Wazo hapa ni kwamba anacho kidonda kikubwa ambacho ngozi mpya haitakua juu yake.

14 Wapenzi wako wote wamekusahau.
17 Yehova aliwangamiza kwa sababu anawapenda na kuwajali watu wake, atawaponya kwa sababu bado anawapenda na kuwajali.

18-21 Nitakufanikisha KATIKA Israeli "mtawala wao" angelikuwa Yesu Kristo (Waebrania 4:16)

Mst.22 Watu wangu! Mungu Wenu

Mst 23-24. Hasira ya Yehova ni sawa na neno lake,halitarudi kwake bure. (Linganisha na Isaya 55:11)

## MARUDIO

**Mstari wa kukariri Yeremia 1:10,7:11,13:23,17:5, 20:9,23:29,29:12**

1:17-19 Unafanya upande wako na Mungu atafanya upande wake.
2:11 Hata mataifa hawabadihishi Mungu wao.
4:27 Mungu daima hushikilia mwanga wa tumaini.
5:6 Ishi sawa na mnyama, kufa kama mnyama.
7:16 Kuna pointi maombi hayawezi kusaidia.
9:9 Kama watu Mungu wangeli fahamu utakatifu wa Mungu, kungelikuwa na wenye kaki wengi Ulimaenguni.
10:5 Muingu hawezi kukudhuru.Wala hawawezi kukutendea mema.
10:24 Tusiposikiliza masahihisho, ghadhabu inakuja.
11:11-13 Maombi ya wasiomcha Mungu hayasikilizwi
14:7 Dhambi zetu zinatushuhudia
18:8-10 Ahadi za Mungu zote ni zenye masharti.
20:4 Tunaweza kuwa hofu kwetu wenyewe na kwa marafiki zetu.
27:12,13 Utumwa ni uzima- kupinga ni mauti.

## SURA 31

**UTARATIBU WA MUNGU MPYA UNAKUJA!**

Mst.10. Ni mchungaji yule yule anayetawanya na kukusanya.

Mst 11. Kuna tofauti kati ya neno <u>"kukombolewa ' na</u>
<u>"kuwekwa huru " = "fidia"</u>

Kukombolewa kunahusika na mkombozi au mtu wa karibu katika familia.
Kuwekwa huru au fidia = "Kununua kilichokuwa chako awali"

Mst 15. Linganisha Mathayo 2:17,18.

Mst 20. Israeli watapokea rehema.
Mst 21. Weka alama njia ya kurudi nyumbani-fanya hivyo sasa! Njia sio mpya! Nikufuata sheria ya Yehova. Kurudia nchi yao kutategemea kurudi kwao kwa Mungu.

Mst.22- Kwa nini? Kwa sababu Yehova ameumba kitu kipya duniani (utaratibu mpya!).
<u>Mke</u> = <u>Isaeli</u>
<u>Mume</u> = <u>Mwana wa Mungu</u>.

Uhusiano mpya umeelezewa katika mst.31-34
Linganisha na Waebania 8:10-13;10:16,17

Mst. 30. WAJIBU BINAFSI! Utateseka kwa ajili ya dhambi zako mwenyewe.

Mst.34. Linganisha Yohana.6:45; Isaya 54:13

Mst.37. Mungu wako ni mkubwa au mdogo kiasi gani? Kama Mungu wako sio Mungu anayekuwa pote na mwenye nguvu zote, Yenye ni mdogo zaidi.

## SURA 32.

Mst.1-5. Sedekia anamtia Yeremia gerezani .

Mst.3 Kama Sedekia angelimsikiliza Yeremia kwa makini vya kutosha, kunukulu maneno kwa usahihi angelifahamu jibu pia!

Ukweli ni kwamba Sedekia haulizi swali,bali anaomba kuokolewa.

Mst6-25. <u>Yehova amtia nguvu Yeremia</u>:
<u>(a) Nunna kiwanja</u>
<u>(b) Ni biashara nzuri katika Yuda</u>

Ununuzi wa kiwanja na kuandikwa kwa habari hizi kunamweka Yeremia afahamike kuwa anadai kuwa kutakuwako na maisha mazuri katika Yuda baada ya uhaimisho.

Mst.16-25. Hii ni sala. - Angalia ni katika mstari mmoja tu ambao ni mstari wa mwisho unadai mambo ya mtu binafsi. Sehemu ya sala yote inamsifu Yehova.

Ni vipi sala katika sala zetu? Ni kiasi gani ni ile inayohusu maisha yako binafsi? Je! Tunajaribu kumtumia Mungu kujibu tu sala zetu binafsi na baada akisha jibu,kufanya kuwa kitu kisicho kuwa na maana maishani mwetu tena?

Mst.37-40. Mungu anatabiri mwisho wakuabudu sanamu.

Mst.41-44. Mwanga wa matumaini umetolewa tena.

**SURA 33.**

**YEHOVA ANAAHIDI BARAKA**

Mst.7. Mateka wa Yuda na Israeli watarudi.

Mst.9. Yuda atakuwa mwaminifu.

Je! Wewe na kusanyiko lako nifuraha kwa Bwana? Au je maisha yenu huyapinga injili? Wakati mwingini adui mbaya sana wa kuzuia kuenea kwa injili ni maisha ya Kanisa. Kuna nafasi kubwa katika makanisa mengi kati ya yale tunayoyafundisha na maisha tunayoishi. Haipashwi Kuwa hivyo. Kama ndivyo ilivyo tutajibu kwa Mungu kama mtu binafsi na kama viongozi.

Mst.14-18. **Kimasihi.**

Tatizo la Israeli lilikuwa lenye sehemu mbili, (I) Wafalme walioshindwa kutenda haki na utawala wa kitauwa na makuhani waliokuwa wameshindwa kuwafundisha watu njia za Mungu.

Kiongozi mpya (Kristo) atafanya wafalme walichopaswa kufanya-kufanya haki usawa.

Kiongozi mpya atachukuwa ofisi hizi mbili kwa pamoja na kuwa Masihi (Kristo) wa Mungu.

Mst.20-21.Matunzo na upendo wa Mungu ni ya uhakika sawa na;
(a). Jua,mwezi,na nyuta.
(b). Mchana na usiku.

Mst.25-26. Uhamisho sio mwisho wa Isaeli kuwa wateule.Watabakia watu wa Mungu hadi kusudi la Mungu nao litakapo kamilika.

Walikuwa watu bwa Mungu Walio chaguliwa kwa kusudi Mbili:

(a).Watunzaji wa mausia Mungu (Agano la Kale) na
(b). Taifa ambalo Masihi angelileta ulimwengani kupitia wao.

**C. DHAMBI YA SEDEKIA NA UTIIFU WAKE KWA WAREKABI**

**SURA 34**

**UHAKI KAWA USHINDI WA BABELI.**

Mst 1-5 Maneno haya yanoonekena kuwa maneno ya "Ikiwa-Ndipo" Ikiwa Sedekia atasikia neno la Bwana,ndipo atakaposhikwa, Ndipo atakufa katika amani. Linganishwa 27:12,13

Mst.10-11. Hali isio aminika ya kuwatatendea watumwa .
Walikuwa wamewaacha huru watumwa wao lakini sasa baada kutafakari kupoteza hali yao ya uchumi,wana rudia vyapo vyao. Kwa nini tuabadu fedha zetu badala ya Yehova? Kuna uzuri gani kuupata ulimwengu wote na kupoteza roho zetu.

Mst.17. Matokeo! Kwa sababu Yuda hawakuwaachia ndugu zao, Yehova ataachilia Upanga, njaa na tauni juu yao.

Mst.18."Kumkata ndama" – Ihiyofanywa kwa sherehe (Lingaisha Mwanzo 15:9,10,17,18, - Abraham na Yehova.

## SURA.35

## UTII WA WAREKABI

Mst1-11 Uthabiti, walikuwa wenye utii wenye nguvu sana.Ni somo la namna gani kwa Yeremia na hata na sisi leo.

Yonadabu.Linganishe na 2 Wafalune 10:15-28.

(a) Alikwenda pamoja na Yehu.
(b) Alitokama na Yethro-Baba mkwe wa Musa

Mst.12-19 Warekabi wanatii- kwa nini wewe usitii?

Mistari hii ni mahimu sana kuhusu maana ya kusikiliza yatakiwayo kwa kusikiliza,nagharama ya kutosikiliza. Kila kitu kitategemea kusikihiza mwisho wake ni kutii.

Inaonekana kwa kawaida kuwa ni kweli kwamba walio maskini, wale walio na uchache vya kupoteza an kupata katika ulimwengu ni wasikilizaji wazuri. Wale walio na vingi vya kupoteza au kupata wanaonekana kuwa watu wasiosikiliza.

## SURA.36.

**Kalamu ya kisu ya Yehoyakimu**.

Mst.2,3. Labda Yuda atatubu.

Mst5-6 Baruku anapaswa kusoma kitabu katika nyumba ya Bwana –Yeremia nimfungwa.

Mst 9-14. Neno la Bwana linatakiwa kutangazwa hadharani. Halipaswi kufichwa.

Yeremia atakwenda isipokuwa ni kupitia Baruku,mfanya neno la Mungu kufamika hadharani.

Mst.15. wakuu wanatake wasikilize wenyewe.

Mst.17,18 ikiwa wakuu watapenda kufahamu uhakika wa maandiko na kufanya jambo jui yake, wanapaswa kufahamu chimbuko na mamlaka yake.

Mst.21 sasa yameletura kwa mfalme.

Mst.23.kutokuamini kwa mfalme.

Mst.25. katika matokeo mfalme,alipokataa gombo, alikataa neno la Mungu lote pamoja na lile lililo husiana na ulinzi kutokana na neno hilo.

Mst.26. hali inakuwa mbaya, fungu la maandiko linaonyesha kwamba majaliwa ya Mungu yameingilia keti kwa ajili ya Yeremia na Baruku.

Mst 27-32. andika tena isipokuwa lifanye kuwa gumu.

Mst 30. unapaswa kufa bila watoto wako kukalia kiti chako cha enzi.
meneno mengi zaidi,nakumzidishia mfalme matatizo.

**E. YEREMIA GEREZANI KIPINDI CHA KUHUSURU ………………….37-39**

## SURA 37

### BABELI WATARUDI NA KUANGAMIZA

Mst.1-3. Sedekia amweka huru Yeremia. Na kusema,"Tuombee"
Je! Sijambo la kushangaza kwamba mfalme huyu aliye`likataa neno la Mungu, kwa haraka anaomba maombi kwa Mungu kwa niaba yake?

Mfalme anahitaji msaada wa nabii sio wa amiri wake. Mtu huyu yako katika hofa kubwa na hali ya kakata tamaa.

Mst 5 Babeli waacha Yerusalemu na kupigana na Misri.

Mst.9,10 Usidanganyike, hata waliojeruhiwa (vilema) wanaweza kukushinda.

Mst 16. Anarudi gerezani.

Mst 17 Je kuna neno lolote kutoka kwa Bwana?

Mst 18-20 Yeremia anamsihi mfalme-Nimethibitika kuwa Nabii wa kweli lakini wewe unanitia gerezani. Lakini manabii wako waliothibitika kuwa manabii wa uongo wanaostahili kifo wako huru. Haki yako iko wapi,Sedekia

.

Mst 19 Manabii wa uongo wako sasa wako wapi?

Mst 21 Sedekia anamhurumia Yeremia. Afungiwe nje na kupata chakula kama kawaida

**SURA 38**

**UOGA WA SEDEKIA**

Mst. 1-4 “Yeremia ni mhaini.”

Gedalia-Mwana wa Pashuri

Mst 4 Yeremia “ hawatafuti heri watu hawa, bali shari yao” katika macho ya nani? Yeremia auawe!

Mst 5 Hakuna “uti wa mgongo” katika Sedekia-anaogopa kusima mbele ya watu.

Mst 6 Akatupwa shimoni!

Mst 7-13 Sedekia anasikia kusihi kwa towashi mkushi kwa kumfungua Yeremia

Mst 11 Ebed-Meleki ni mtu mwenye huruma. Hata analeta nguo kutuliza maumivu yalisababishwa na kamba walizomteremshia shimoni.

Mst 15 Yeremia anamfahamu Sedekia.

Mst 14-28 Mwisho uko hapa.

Mst 19 Sedekia hafai kutawala anavyohitaji “mawazo ya watu”kabla hajatoa maamnzi. Anaogopa watakachokisema watu.

**SURU 39**

**UNABII UNATIMIZWA!**

Mst 1-3 Baada Yerusalemu kuhusuriwa kwa miezi 18, ilianguka.

Mst 4-7 Sedekia:

(a) Anatoraka …………………………………...mst 4

(b) Anashikwa…………………………………..mst 5

Hukumu ya Sedekia kutoka kwa Mungu inatekelezwa:

©Kuwaua kwa wanawe mbele yake……………...mst 6

d.Ondoa macho yake……………………………..mst 7

Kumbuka kitu cha mwisho ulicho kiona!

Mst.8-10 Kazi ya Nabuzaradani (linganisha na 2Wafalme 25:8-19)

a. Unguza Hekalu

b. Unguza Jumba la Mfalme

c. Unguza nyumba za wakuu wake

d. Vunja kuta za mji

e. Ondoa mateka

f. Acha masikini kutunza mashamba

g. Kuchukua vyote vyenye thamani toka nyumba ya Bwana (vilirudi baada miaka 100)

h. Ondoa makuhani wakuu

i. Ondoa wanaume wa vita

Mst.11-14. Yeremia anatendewa vizuri sana

a. Anapewa uhuru wa kwenda apendako

b. Anapewa vitu walivyoteka

c. Anapewa zawadi

Mst.15-18 Ebed-Meleki anazawadiwa kwa wema wake.

a. Hutaanguka mkononi mwa wale unaowahofu.

b. Hutawaua

**III. Unabii baada ya kuanguka kwa Yerusalemu………….Sura 40-45**

**A. Huduma kati ya mabaki katika Yuda…………….Sura 40-42**

## SURA 40

**Matatizo zaidi nyumbani.**

Mst.1-6 Amiri wa askari atambua kuwa ni kazi ya Mungu "Bwana Mungu wako"

Yeremia anapewa uhuru wa kuchagua pa kwenda.

Mst. 7-8 Jeshi la Kiyahudi lililokuwa limetawanyika linarudi.

Mst.9-12 Gedalia anawambia kuishi salama na Babeli.

Mst.13-16 Gedalia anaelezewa njama za Waishimaeli(Ammonites) za kumua.

Lakini hakuamini.
Mst.15 Yohana anasema, kwa nini mabaki waangamie?

---

## MARUDIO

**Mstari wa kukariri Yeremia 1:10,7:11,13:23,17:5, 20:9,23:29,29:12,51:7**

1:17-19 Unafanya upande wako na Mungu atafanya upande wake.
2:11 Hata mataifa hawabadihishi Mungu wao.
4:27 Mungu daima hushikilia mwanga wa tumaini.
5:6 Ishi sawa na mnyama, kufa kama mnyama.
7:16 Kuna pointi maombi hayawezi kusaidia.
9:9 Kama watu Mungu wangeli fahamu utakatifu wa Mungu, kungelikuwa na wenye kaki wengi Ulimaenguni.
10:5 Muingu hawezi kukudhuru.Wala hawawezi kukutendea mema.
10:24 Tusiposikiliza masahihisho, ghadhabu inakuja.
11:11-13 Maombi ya wasiomcha Mungu hayasikilizwi
14:7 Dhambi zetu zinatushuhudia
18:8-10 Ahadi za Mungu zote ni zenye masharti.
20:4 Tunaweza kuwa hofu kwetu wenyewe na kwa marafiki zetu.
27:12,13 Utumwa ni uzima- kupinga ni mauti.
31::31 Utaratibu wa Mungu mpya unakuja. Linganisha na Ebra.8:10-13;10:16,17

---

## SURA 41

**Utawala wa Waamoni unapingwa.**

Mst.1-3 Ishimaeli watu wake 10 walimuua Gedalia na wengine wengi

Mst.4-9 Ishimaeli pia anawaua 70 waliokuwa waaminifu kwa Yehova.

Mst.10 Ishimaeli anawachukua mateka na kuanza safari ya kwenda Amoni.

Mst.11-16Yohana anasikia kuhusu udanganyifu huu, anaingilia kati ya kundi la Waishimaeli na kuwarudisha watu wote waliokuwa wametekwa.

Mst.17,18 Wote wanakimbilia Babeli kwa kuhofia Babeli.

**SURA 42**

**Unafiki**

Mst.1-6 Yohana na watu wengine wanataka cha kufanya ili wamwendee Yehova.
Soma Mst.5,6
Linganisha na 20-22

Mst.7-12 Baada ya siku kumi Yehova anajibu.

Mst,10 Yehova anawajibu kwa kusema, wabakie na wastawi.

Mst.11 Msiogope.

Mst.13-18 LAKINI mkisema HAPANA!

Mst.15-17 Yohana ukienda Misri:

a. Ulichokihofu kitakuteka……..mst. 16
b. Njaa…………………………..mst. 16
c. Upanga…………………………mst. 17
d. Tauni…………………………...mst. 17
e. Hakuna atakayerudi…………….mst.17

Wauhamisho walio wengi wanafikiria siku moja waturudi katika nchi yao. Lakini Yehova anawaambia kwamba nafasi ya pekee ni kubakia. Lakini wakienda Misri hawatarudi. Vita vitawafuata na kwa hiyo wataangamizwa.

Mst.18. Hivi ndivyo mtakavyo kuwa:

a. Apizo
b. Ajabu
c. Laana = apizo
d. Aibu = ajabu

Mst.19. Msiende Misri! Ni sehemu gani ya amri hii wanayoielewa? Kwa nini wanang'ang'ania kufanya mapezi yao?

Mst.20-22Unafiki mioyoni = maangamizi

Linganisha na mst. 5,6; Galatia 2:11-13

Watu hawa wana matatizo mawili:

a. Wamevunja kiapo chao

b. <u>Na kuvunja amri ya moja kwa moja kutoka kwa Yehova.</u>

B. Huduma kati ya waliotorekea Misri………………Sura 43,44

**SURA 43**

**Watu wanaamini wanachotaka kuamini**.

Mst.2,3 Wanadai Yeremia aliwadanganya.

Mst.4-7 Yohana anamchukuwa Yeremia na mabaki na kwenda Msri.

Mst.8-13 Yeremia anaambiwa na Yehova kuficha mawe mlangoni pa nyumba ya mfalme. Na kuwambia, "Babeli inakuja"

**SURA 44**

**Tutafanya kinachotofurahisha.**

Uaminifu kwa Yehova unapaswa kuwa wenye nia moja sio ya udanganyifu. Yuda haijaonyesha uaminifu usio na uelekevu mmoja.

Mst. 1-6 Yeremia anawakumbusha sababu ya kuanguka kwa Yuda.

Mst. 7-8 Kwa nini ujikatee?

Mst. 15-17 Tutafanya inavyotupendeza.

17. Machoni pao walikuwa na mafanikio na amani walipoabudu miungu, na walipoacha walipatwa na umaskini na vita. Na hawa miungu mke walikuwa na uwezo wa kutunza ahadi zao. Huu ni ubishi mkamilifu machoni mwao wa kuwafanya kuendelea kuabudu miungu.

    Sasa swali linakuja, ni Mungu gani aliye na uwezo wa kulaani na kubariki? Yeremia hakuwaficha ukweli kuhusu jambo hili bado ushahidi kamili unakuja.

Mst. 27,28 Matokeo na mwanga wa matumaini.

Mst.29,30 Ishara- Ikiwa Babeli itatawala, vitisho vyangu vitakuwa vya kweli.

C. Baruku anatiwa nguvu…………………………………..Sura 45

## SURA 45

**Baruku + Yehova = Mafanikio**

Mst. 1-5 Usijitafutie mambo makubwa.

Sura hii nzima ni mausia ushindi kwa Baruku, na wote wanampenda. Umetunza imani na kuwa mtiifu, kwa hiyo utaishi.

Baruku akiendelea kuishi ni ushahidi kwa wa uhamisho kwamba Mungu atatunza ahadi yake kwao pia.

Hii pia inaonyesha kuwa mbele ya utabiri unaoonyesha maafa, bado kuna matumaini.

IV. Unabii kuhusu mataifa ya kipagani………………………………….Sura 46-51

Sura zifuatazo zinafanya matangazo: YEHOVA NI MFALME!

A. Misri……………………………………………………………Sura 46

**Mungu anatawala mataifa yote. Analo kusudi na kila taifa . Hata kama wanajua au hata kama hawajui watahudumia kanuni yake ya haki Wakishindwa, wataadhibiwa na hata kukoma kuwapo kama taifa.**

## SURA 46

Mst. 2. Misri inashindwa katika mwaka wa 605 K.K.

Mst. 10. Yehova anashinda jeshi la Wamisri kana kwamba ni dhabihu ya damu.

Mst. 13. Unabii juu ya Misri unarudiwa

Mst.27,28. Mwanga wa matumaini. Lakini, bado utaadhibiwa.

Yehova anatawa hata Misri vile vile na mataifa mengine. Yehova ataadhibibu Misri, sio kwa sababu anapenda Israeli, bali kwa sababu atawaadhibu wote wasio mheshimu. Yehova akiheshimiwa Israeli atafaidika.

B. Wafilisti…………………………………………………Sura 47

**SURA 47**

Mst. 4. Ni vita vya Yehova.

Mst. 6,7 Upanga hauwezi kuondolewa, - Hukumu inakuja.

C. Moabu……………………………………………………Sura 48

**SURA 48**

Mst. 10. Amelaaniwa mtu yule afanyaye kazi ya Bwana kwa ulegefu

Mst. 11-13 Moabu wanaishi katika starehe- ardhi nzuri…………………..mst.11

Vyote vilivyomo vyomboni vitamwagwa na vyombo kuvunjwa.mst 12

Wataibika kwa sababu ya miungu yao ya uongo sawa sawa na vile Israeli waliaibika kwa sababu ya miungu yao. Mst. 13
Linganisha na Sefania 1:12

Mst. 25. Pembe = mkono= Nguvu

Mst. 29. Kiburi, ufidhuli na dharau husababisha hasara na huzuni.
Linganisha na Yakobo 4:8-10; Mithali 16:18,19

Mst. 46. Ole juu ya Moabu.

D. Amoni, Edomu, Damascus, Arabia, Elamu……………Sura 49

**SURA 49**

Mst. 1-6 Hukumu juu ya Amoni.

Mst. 7-22 Hukumu ya Yehova juu ya Edomu:

a. Edomu hawatakwenda bila kuadhibiwa………………mst. 12

b. Mji wa Edomu kuharibiwa………………………………mst. 17

Mst.12. Kuna ujumbe muhimu hapa. Wasio na hatia hupatikana katika matatizo ya kisiasa yanayowazunguka. Wasio na hatia na wale walio na hatia wote wanateseka kutokana na vita na majanga ya asili. Lakini haina maana kwamba Mungu hawaangaikii. Tunapaswa kukumbuka kwamba Mungu hawafuniki walio wake na majanga kama haya. Kama angelikuwa anafanya hivyo, wengi wangefanyika wakristo siku hizi kwa kutafuta

faida ya kidunia sio kwa sababu wanampenda na kutaka kufanya mapenzi yake.

Mst. 18 Miji jirani ni ile: Adma, Seboimu(Kumb. 29:22,23).
Soari uliachwa kwa ajili ya Lutu (Mwanzo 19:23-25)

Mst. 23-27 Hukumu ya Yehova juu ya Dameski (Ashuru).

Mst.28-33 Hukumu ya Yehova juu ya Kedari (Arabia)

Mst.34-39 Hukumu ya Yehova juu ya Elamu.

E. Babeli………………………………………………………Sura 50,51

Ikiwa Yehova atathibitisha ukuu wa utawala wake juu ya mataifa, Babeli ingelikuwa mahali pake pa majaribio. Ikiwa anaweza kutawala Babeli na uwezo wake jinsi alivyo, basi anao uwezo wa kutawala mataifa mengine yote yaliyopo.

Tukifika mwisho wa kitabu cha Yeremia hatutakuwa na Babeli na Yehova, bali ni Yehova peke yake, Babeli itakuwa imekwisha malizika.

Hatimisho ni kwamba, historia katika hali yake ya mwisho sio mambo ya siasa na nguvu.

Kinacho onekana ni kwamba, Yehova ni Mungu na Mfalme. Wote wanapaswa kumchukulia hivyo na mataifa yote kwa sababu siku ya kutoa hesabu inakuja. Kama sio hapa duniani, itakuwa katika siku ya mwisho.

**SURA 50**

Mst.1-4 Hukumu ya Yehova juu Babeli(Shamu). Wamedi wanakuja. Yehova anawaandaa maadui wapya dhidi ya Babeli, na kwa hiyo Babeli itashindwa.

Mst.4 Israel and Judah will repent.

Mst.6-8 "Mababeru" watakuwa viongozi wenye nguvu wanaopaswa kuongoza Yuda kurudi Yeresalemu. Kurudi kutahiji kujipa moyo mkuu na kwa hiyo, kutahiji uongozi wenye nguvu.

Wayahudi kwenda uhamisho na Wayahudi kurudi kutoka uhamisho ni watu wawili tofauti. Bado ni Wayahudi wale wale lakini tofauti. Israeli ya kale haipo imekwenda, Israeli mpya iko tayari kumtumikia Yehova.

Mst.17-20 Ashuru na Shamu walipata hukumu yao.

Mst.33-34 Yehova ndiye mkombozi wao! Yehova ndiye Mungu wao.

Mst.35-40 Hata wenye nguvu kama Babeli wanaweza kutarajia kupokea hali inayofanana na sera zao.

Mst.39 Kushinda kumekamilika

SURA 51

Adhabu ya Babeli/Israeli na Yuda haijasauliwa.

Mst. 2. "Wapepeaji" watakuja kuhukumu na kuangamiza nchi.

Mst. 7. Nafasi hutoa uajibikaji. Au Uajibikaji hutoa nafasi.

Mst. 9. Mstari huu unaonekana kuoelezea wale wa uhamisho kuondoka kwa sababu matatizo hayawalengi wao.

Mst. 35-37 Yehova atawatetea Israeli na Yuda.

Mst. 45. Linganisha na Ufunuo 18:4

Mst. 47. Miungu wa uongo hawataachiliwa. Linganisha na Kutoka 12:12

Mst. 50,51. Wayahudi waliobaki wanaambia kukumbuka Yerusalemu, kukumbuka Hekalu, wakumbuke kuwa wao wako uhamishoni. Haya yote yalipaswa kuwapeleka Yerusalemu. Wanatakiwa kuanzisha upya Ibada ya Yehova utaratibu wa utawala wake.

Mst. 59. Seraya, kama Baruku ni mwana wa Maaseya, kwa hiyo inachukuliwa kuwa walikuwa ndugu.

Mst. 61-64 Taifa linalozama. Pamoja na matendo haya, na unabii wa Yeremia wana uhamisho wanaweza sasa kuchukulia kwamba muda umefika wa taifa kuonyesha utii wake. Hawataendelea kufungwa na Babeli.

**V. Nyongeza ya Kihistoria…………………………………………..Sura 52**

**SURA 52**

**Sedekia/ Yerusalemu/Yehoyakimu**

Mst. 1-11 Uasi na kushindwa kwa Sedekia (mfalme wa Yuda wa mwisho). Huu ndiyo mwisho wa utawala wa Daudi. Mwana wa Konia hatakalia kiti akiwa Yerusalemu na kufanikiwa. Linganisha na 22:24-30

Mst. 12-30 Kuharibu hekalu na watu.

Ingawaje watu wengi walipelekwa uhamishonin, Nebukadraza aliacha watu wakutosha kutunza ardhi ili lisibakie bila watu kabisa. Huu ni utaratibu mzruri wa kivita. –Usiharibu watoa kodi kabisa.

Kuondoa vyombo vya hekaluni vyote ni kuondoa uwezekano wa Waliobaki kuita hili kuwa hekalu la Yehova. Hii pia inaonyesha kwamba Mungu alikuwa amefanya ibada katika hekalu hii kukoma.

Mst. 28-30 Ingawa namba hii inaonekana kuwa kubwa, lakini ni ndogo ukilinganisha na taifa zima la Yuda.

Mst. 31-34 Yehoyakini anapewa heshima uhamishoni.

Yehoyakini = Yekonia = Konia

## Yeremia Kihistoria:

Yeremia alitabiri kipindi cha wafalme watano wa Yuda:

1. Yosia (639-608) - miaka 31
2. Yehoyahazi (608 K.K.) -miezi 3
3. Yehoyakimu. (608-597) K.K. -miaka 11
4. Yehoyakini. (597 K.K.) -miezi 3
5. Sedekia (597 K.K.) -miaka 11

Nabii Yeremia alianza kutabiri katika mwaka wa 13 kwa utawala wa Yosia (626 K.K.) Alimaliza kazi yake katika mwaka wa 586 K.K. pale Yerusalemu ilipoanguka. Lakini aliendelea kufanya kazi hadi mwaka wa 560 K.K. Jumla ya miaka 66 tukisoma sehemu ya nyongeza katika Sura ya 52:31. Hii ni miaka 26 baada ya kuanguka kuanguka kwa Yerusalemu.

Hali maisha kipindi cha Yeremia:

Baali aliabudiwa na madhabahu ya kipagani yalijengwa.

Watoto walitolewa kama dhabihu ya kuteketezwa.

Ibada ya jeshi la mbinguni ilianzishwa.

Manabii waliteswa.(mapokeo yanatujulisha kwamba Isaya alikatwa na msumeno) (Waebrania 11:37)

**Masomo tunayopata katika kitabu cha Yeremia:**

1. Kitabu kinazungumzia Mungu:
    a. Kuwa pote kwa Mungu.
    b. Ufahamu wa mambo yajayo
    c. Alijua tabia za nabii hata kabla hajamwita
    d. Uwezo alionao hata kabla hajazaliwa

    Muumba ataheshimu uhuru wa mtu lakini anafahamu. Kwa kuwa yeye ni Mungu.

2. Mtu akiwa tayari kutumiwa na Yehova:
    a. Mungu anaweza kubadilisha unyonge wake na kumfanya kwenye nguvu. (Yeremia alikuwa mwoga lakini alibadilishwa kuwa hodari)

3. Mtu akisahau kiapo chake cha mwazo kwa Mungu na kuanza kufuata yale ambayo hajaambiwa, hutenda dhambi.

4. Dini ya nje bila kupenda Mungu kwa moyo haifai

5. Toba ya kweli ni kuacha uovu na kumfuata Yehova.

6. Dhambi ina gharama kubwa. Inaharibu kwa ndani, kwa nje, na hata milele.

7. Haki ya Mungu itashinda uovu. Ukweli unaokanyagiwa chini, utainuka tena.

8. Matumaini ya pekee ni kupitia Masihi na agano lake.

9. Wanaokataa kukubaliana na dhambi, watateseka.

10 Kila mtu bila shaka ata simama mbele ya hakimu wa ulimwengu.

**Yeremia na Akiolojia**

Kuna vitu vingi walivyovichimbua wanaakiolojia vyenye habari ya kitabu cha Yeremia. Kuna mfano wa baadhi yake.

1. Kati ya mwaka wa 1935-1938 vipande vya vigae ishirini na moja (vilioitwa Ostraca) viligududuliwa mahali palipokuwa mji wa zamani Lakishi (Maili thelathini kusini magharibi mwa Yerusalemu.

    a. Lakishi ulikuwa moja wapo ya miji mitatu Nabukadreza alizotakiwa kuteka.
    (Linganisha na Yeremia 34:7)

    b. Maandishi haya yalipatikana katika vyumba vidogo vya ulinzi nje ya lango

la mji yakiwa yameandikwa katika lugha ya Kiebrania.(589 K.K.)

c. Baadhi ya vipande vile vilikuwa na maandishi ya barua iliyotoka kwa moja ya askari akimwandikia mkuu wake kule Lakishi inayosema, “Kuna wakuu Fulani wanaotudhoofisha mikono yetu” Hii ni sawa na mashitaka waliokuwa wakimshitaki Yeremia. (Linganisha na Yeremia 38:4)

2. Baada ya kuanguka kwa Yerusalemu, Gadelia alichanguliwa na Nabukadreza kuwa liwali katika Yuda makao makuu yake yakiwa Mizpah.(2Wafalme 25:22-26;

Yeremia 40:5-41:8)Katika magofu ya mji wa Lakishi kuliguduliwa jagi yenye maandishi, “Gedalia mkuu wa nyumba” Huyu inawezekana alikuwa Gedalia wa kitabu cha Yeremia. Katika misiamu kule Ungereza kuna maandishi yaliyopatikana ya karne ya sita K.K. yenye maandishi, “mali ya Hannania mwana wa Gedalia.

3. Yeremia anataja kwamba Yehoyakini mfalme wa Yuda, aliyekuwa mateka kule Babeli alitendewa “vema” (Yeremia 52:31-34). Maandishi juu ya vibao vya udongo vilipatika katika magofu ya mji wa Babeli vikiwa na maandishi, “Yehoyakini alitendea vema na wakuu wa Wakalidayo. Anatajwa kama “Yaukin, mfalme wa Yuda.”